

**MWINYI:** Haya ndiyo yalinifanya nisiwaajiri wahitimu wa vyuo vikuu

UKURASA 3

**WALIOSAMEHEWA** na Rais wauawa kikatili kwa kipigo

UKURASA 3


Nipashe TESA
Jumanne Mei 11, 2021 TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 14 Mbinu udhibiti uharibifu wa vifaa umeme hizi

Ukurasa 12 Wenye ulemavu kumekucha mkopo Manispaa wawapaisha

Ukurasa 13 Vigingi hivi vinawakwamisha wanaojifungua kurudi shuleni

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

Ndivyo Tanzania ilivyobahatika kuviepuka vimbunga na tufani

LICHA ya kimbunga cha kitropiki cha jobo kuelezwa kuwa kingepiga pwani ya Tanzania na kusababisha maafa ukanda wa pwani, taarifa za watabiri wa hali ya hewa kimataifa zinasema ni nadra kutokea tufani hizo kwa vile Tanzania si mkondo wa vimbunga.

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), mwezi uliopita taifa lingeandika historia, ni ya kimbunga jobo ambacho kingeipiga Zanzibar, Mafia, Dar es Salaam na mikoa ya Lindi na Mtwara.

Kuhusu kimbunga hicho kutofika nchini, ilielezwa kuwa ni Tanzania si ukanda wa tufani za baharini kwa kuwa iko karibu na Ikweta ambao ni mstari wa 'kufikirika' unaoitenganisha dunia katika vipande viwili, kizio cha Kaskazini na cha Kusini.

Athari za kimbunga katika baadhi ya miji duniani. PICHA: MTANDAO

kubwa zaidi kwa kufika nchi kavu hasa mikoa ya ukanda wa pwani.

Hofu ya kukumbwa na kimbunga hicho kilichotangazwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilikuwa kubwa zaidi kwa wakazi wa mikoa ya ukanda wa pwani ya kusini inayohusika mikoa ya Lindi na Mtwara. Aidha, kilitarajiwa kufika Zanzibar, Bagamoyo pamoja na Dar es Salaam.

Hata hivyo, hofu ilitoweka baada ya kimbunga jobo kilichotarajiwa kilichokuwa kiwasili nchini Jumapili Aprili 25, kutangazwa na TMA kuwa kilitoweka na hakipo tena kutokana na kupungua nguvu na kufifia wakati kilipowasili katika ukanda mkavu wa pwani ya Tanzania.

ATHARI ZA VIMBUNGA


# Nipashe

Jumanne Mei 11, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580577

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


UKURASA 11

# Serikali yatoa tamko sakata Simba, Yanga

**KAMATI** ya Saa 72 yajifungia kumsaka 'mchawi', wizara nayo...

*Endelea Ukurasa 2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza Bungeni jijini Dodoma, jana, kuhusu maagizo ambayo ameyatoa kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, juu ya sakata la kuahirishwa kwa mechi ya Simba na Yanga, iliyopangwa kuchezwa Uwanja wa Mkapa Dar es Salaam, Mei 8, 2021. Kushoto ni Mbunge wa Makambako, Deo Sanga. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

### WAWEKEZAJI ZAIDI WAJA KUMALIZA UHABA SUKARI

SERIKALI imetoa ardhi kwa wawekezaji 14 katika mikoa minne, ikiwamo wawili watakaojenga viwanda vya sukari Morogoro na Kigoma ili kukabiliana na tatizo...

**UKURASA WA 5**

### NSSF YAPANIA KULIPA WANACHAMA KWA WAKATI

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, amemhakikishia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na...

# Uhakiki wa taasisi za dini waanza kurindima

UKURASA 2

## Tundu Lissu: Sijajibiwa na serikali

UKURASA 2

**MICHEZO** GOMES AELEZA JEURI USHINDI KAIZER CHIEFS UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

**HABARI KITAIFA**

## SAKATA SIMBA, YANGA

# Serikali yaingilia hatima viingilio

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amelazimika kulizungumzia bungeni sakata la kuahirishwa kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya watani wa jadi, Simba na Yanga, iliyokuwa ichezwe Jumamosi.

Ameweka wazi kuwa tayari serikali imeitaka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoa taarifa haraka kuhusu hatima ya viingilio vya mashabiki na mechi yenyewe.

Majaliwa alisimama bungeni jana asubuhi kuzungumzia suala hilo baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali' na kuomba kutoa ufafanuzi kwa Watanzania na washabiki wa mpira wa miguu kuhusu kero hiyo iliyoibua mjadala mkali wa kitaifa.

"Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kufuatia kero iliyojitokeza Mei 8 (Jumamosi), tukio lililowakera sana wanamichezo hasa wapenda michezo nchini baada ya kuahirishwa kwa mchezo wa watani wa jadi, Simba na Yanga uliotakiwa kuchezwa siku hiyo na kusababisha manung'uniko, mijadala kwenye mitandao ya kijamii, lakini kutojua hatima ya waliolipa viingilio kwenye mchezo huo.

"Jambo hili limevuta hisia za Watanzania hata pia nje ya nchi, kwa sababu timu hizi ndiyo zimebeba image (taswira) ya michezo hasa mpira wa miguu Tanzania," alisema.

Majaliwa alisema kuwa kutokana na kero hiyo, wizara husika imeagizwa kuhakikisha inatoa taarifa sahihi na haraka kwa Watanzania kuwa mchezo wenyewe utachezwa lini na nini hatima ya viingilio vya wananchi walioingia kwenye mchezo huo.

"Niwasihi Watanzania na hasa wapenzi wa michezo kwenye eneo la mpira wa miguu ambao pia walijiandaa kuona na kusikia, lakini walitoa viingilio kwamba tuipe muda wizara ije kutoa taarifa kwa kushirikiana na taasisi za michezo ili Watanzania wapate kujua hatima kuhusu hayo niliyoeleza," alisema.

Mchezo huo ulioahirishwa katika mazingira yaliyozua utata kutokana na mabadiliko ya muda wa awali ambao ulipangwa kuwa saa 11:00 jioni Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) ikatoa taarifa ya kubadili muda wa kuanza kwa mchezo huo hadi saa 1:00 usiku siku hiyo.

**KAULI YA TPLB**

Katika taarifa yake ya jana, TPLB ilibainisha ratiba iliionyesha mchezo huo ulipangwa kuanza saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Mkapa, lakini ilipotimu saa saba mchana siku hiyo, ilipokea maelekezo ya mabadiliko ya muda wa kuanza kwa mechi hiyo kwamba uanze saa 1:00 usiku kutoka Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Bodi hiyo ilibainisha kuwa ilitekeleza maelekezo hayo kwa mujibu wa kanuni zinazoongoza zinazoitaka itii maelekezo ya Shirikisho la Soka Ulimwenguni (FIFA), Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF) na TFF.

"Kupitia taarifa hiyo, timu zilipewa taarifa rasmi ya mabadiliko na ikatangazwa kwa washabiki waliokuwa ndani ya uwanja na kuwekwa machapisho kwenye kurasa za mitandao ya kijamii ya TFF na bodi, ikiwa ni wastani wa saa tatu kabla ya muda wa kikanuni wa timu kuwasili uwanjani kwa ajili ya mchezo wa saa 11:00 jioni," ilibainisha.

Ilibainisha kuwa Sekretarieti ya TPLB imeshapokea taarifa zote kuhusiana na mechi hiyo kutoka kwa maofisa mbalimbali wakiwamo makamisaa na mwamuzi kwa mujibu wa kanuni za ligi.

Kutokana na tatizo lililojitokeza la mchezo huo kuahirishwa, bodi hiyo ilibainisha Kamati ya Saa 72 ilitarajiwa kukutana, pamoja na mambo mengine, kuujadili mchezo huo.

Tangu kutokea kwa utata katika kuahirishwa kwa mchezo huo uliovutia washabiki kutoka ndani na nje ya mipaka ya Tanzania, uongozi wa TFF chini ya Rais, Wallace Karia, umekuwa ukisisitiza uliagiza TPLB kubadili muda wa kuanza kwa mchezo huo kufuatia maelekezo ya serikali.



Balozi mpya wa Uturuki nchini, Dk. Mehmet Gulluoglu (kulia), akiwasilisha hati za utambulisho kwa Rais Samia Suluhu Hassan Ikulu jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula pamoja na viongozi wa serikali. **PICHA: IKULU**

# Uhakiki taasisi za dini kuanza kurindima

**Na Elizabeth Zaya**

UHAKIKI wa taasisi za kidini na jumuiya za kijamii katika Kanda ya Magharibi utaanza Juni 6 hadi 16 mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye vyombo vya habari jana na Msajili wa Jumuiya za Kijamii, Emmanuel Kihampa, hiyo ni awamu ya sita kufanyika kwa uhakiki huo.

Mikoa itakayohakikiwa katika awamu hiyo ni Tabora, Kigoma na Katavi.

Kwa mujibu wa Kihampa, miongoni mwa nyaraka zitakazohitajika wakati wa uhakiki ni cheti halisi cha usajili na kivuli cha cheti hicho, stakabadhi za malipo ya ada kwa miaka ya nyuma, katiba na kanuni za jumuiya au taasisi husika zilizopitishwa na msajili pamoja na vivuli vya nyaraka hizo.

Nyingine alisema ni barua inayothibitisha uwapo wa jumuiya au taasisi husika kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Mtaa au kata ilipo ofisi taasisi au jumuiya husika, taarifa ya mkutano mkuu wa mwaka na taarifa za fedha ya mwaka.

"Taasisi ambazo zitashindwa kuhakikiwa kwa mujibu wa ratiba ya eneo husika zitalazimika kwenda ofisi ya Msajili wa Jumuiya za Kijamii jijini Dodoma kwa ajili ya uhakiki. Iwapo zitashindwa kwa muda uliopangwa zitaondolewa kwenye rejista ya jumuiya zilizosajiliwa," alisema Kihampa.

"Kwa upande wa taasisi na jumuiya hizo ambazo bado hazijasajiliwa, viongozi wao wanatakiwa kufika wakati wa zoezi la uhakiki kwa ajili ya kupewa utaratibu wa kujisajili. Utaratibu huu unahusisha taasisi za kidini zilizosajiliwa katika bodi ya wadhamini pasipo kusajili taasisi husika katika ofisi ya msajili wa wizara husika."

"Sambamba na uhakiki, Ofisi ya Msajili itatoa elimu kwa umma juu ya aina ya vikundi na vyama vinavyopaswa kusajiliwa, umuhimu wake kwa vikundi hivyo na masharti yanayopaswa kuzingatiwa."

# Lissu: Serikali haijanijibu

**Na Enock Charles**

MAKAMU wa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema bado anasubiri majibu ya Rais Samia Suluhu kuhusu ombi lake la kuongea naye huku akiendelea kusisitiza kuhakikishiwa usalama ili kurejea nchini.

Lissu ambaye bado yupo ughaibuni tangu kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana, amesema hawezi kurejea nchini kwa sasa kwa kuwa anaona bado waliotaka kumuua mwaka 2017 hawajachukuliwa hatua.

"Ombi langu halijajibiwa bado halijajibiwa, kurudi kwangu kunategemea serikali yake (Rais Samia) ina mpango gani na usalama na uhuru wangu," Lissu alisema katika mazungumzo na Nipashe kwa njia ya mtandao juzi.

Mtaalamu huyo wa sheria aliendelea: "Hayo ni mambo muhimu kwangu, serikali itakapoyatolea ufafanuzi na kunipa assurance (uhakika) juu ya masuala hayo, basi nitarejea nyumbani."

Alipotafutwa na Nipahe jana kuzungumzia hoja hizo za Lissu, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema suala la serikali ama kukubali au kukataa kuongea na Lissu litabainishwa kwa Lissu mwenyewe na si kwa chombo cha habari.

"Majibu atapewa yeye mwenyewe muhusika (Lissu), siyo kazi yenu kufuatilia mawasiliano ya Ikulu," Msigwa alisema.

Septemba 7, 2017, Lissu alishambuliwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana wakati anajiandaa kushuka kwenye gari lake, nyumbani kwake Area D mjini Dodoma, alipokuwa anatoka bungeni kushiriki kikao cha Bunge ambacho alichangia hoja siku hiyo.

Baada ya kukaa ughaibuni kwa kipindi kirefu akidai kupatiwa matibabu ya kibingwa Ubelgiji, mwanasheria huyo ambaye amehudumu kama mbunge kwa karibu mihula miwili, alivuliwa ubunge baada ya Spika Job Ndugai kubainisha kuwa ni mtoro na hakujaza fomu za maadili ya watumishi wa umma ambazo hutakiwa kujazwa pia na wabunge wote.

Mwaka jana, Lissu alichaguliwa na chama chake kushika nafasi ya Makamu Mwenyekiti katika uchaguzi uliofanyika Mlimani City, Dar es Salaam huku yeye akishuhudia kwa njia ya mtandao akiwa Ubelgiji na katika hali isiyotarajiwa na wengi mwaka huo huo alirejea nchini na chama chake kumpitisha kuwa mgombea wa nafasi ya urais kupambana na Hayati Dk. John Magufuli.

Baada ya Uchaguzi Mkuu ambao hakufanikiwa kushinda, Lissu alirejea tena Ubelgiji kwa madai ya kutishiwa maisha yake huku pia chama chake kikitangaza kutoridhika na matokeo ya uchaguzi kwa madai ya kufanyiwa hujuma.

HABARI KITAIFA

# Mwinyi: Haya yalinifanya nisiajiri wahitimu wa vyuo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amekumbusha alivyolazimika kutokuwaajiri wahitimu wote wa vyuo kutokana na hali mbaya ya kiuchumi.

Katika kitabu chake cha 'Mzee wa Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anabainisha uamuzi huo aliuchukua mwaka 1989/90 wakati serikali yake ilipoangalia upya vipaumbele vya matumizi ya serikali.

Anasema wabunge pia waliitaka serikali yake ipunguze matumizi yasiyo ya lazima, ndipo akaamua kuchukua hatua kadhaa ikiwamo ya kutowaajiri wahitimu wote wa vyuo vikuu. Kipindi hicho, wahitimu wote walikuwa wanaajiriwa mara moja baada ya chuo.

"Kwa mara ya kwanza serikali ikasema haitaajiri kila anayemaliza masomo ya chuo kikuu, isipokuwa kwa sekta kama afya, elimu na taaluma kama vile wahandisi na wahasibu. Mwaka huo, kati ya wahitimu 552, tuliajiri 99 tu," anasema.

Mwinyi anataja hatua zingine zilizochukuliwa kuwa ni pamoja na kuwapunguza wafanyakazi 310 wa Shirika la Ndege Tanzania ambalo lilikuwa halifanyi vizuri na ofisa zao sita ndani na nje ya nchi zikafungwa.

"Serikali ilisitisha uhamisho wa watumishi wa umma, isipokuwa kama ni lazima sana na kupunguza siku za mtumishi kuwa nje ya kituo chake cha kazi kutoka siku 84 hadi 60 tu kwa mwaka.

"Serikali ilikataza safari za ndege isipokuwa kwa kibali maalum, tena kwa maandishi.

"Ofisi zetu za ubalozi nchini Sudan na Guinea zikafungwa na serikali ikafuta utaratibu wa kuwalipia ada za shule watoto wa watumishi kwenye ofisi za ubalozi nje ya nchi wasomao sekondari na kuendelea.

"Semina kwenye serikali na mashirika zikapunguzwa, idadi ya magari kwenye misafara ya viongozi mikoani nayo ikapunguzwa sana," anasema.



Naibu Waziri wa Nishati, Steven Byabato, akisikiliza maelezo kutoka kwa kiongozi wa zamu wa kituo cha kupoza umeme cha Mtera, Asanterabi Mngulwi, kuhusu kituo hicho kinavyofanya kazi ya kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali, wakati wa ziara ya kikazi iliofanyika jana ya kutembelea bwawa la Mtera hilo. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Bili za maji kulipiwa kama luku za umeme

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema wanakamilisha utaratibu wa kufunga bili za maji za matumizi kabla (pre paid bill), huku akiagiza wabunge wote kufungiwa huduma hiyo.

Akijibu hoja mbalimbali za wabunge jana, alisema walianza kwa kufunga mita Bandarini na kuongeza makusanyo kutoka Sh. milioni 20 hadi Sh. 103.

"Utaratibu huu utaongeza makusanyo na kushughulikia suala la kubambikia bili, naagiza wabunge wafungiwe mita za malipo kabla," alisema.

Aidha, alisema wamefukuza waandishi 118 kutokana na kushindwa kutimiza wajibu wao na ubadhirifu, huku wahandisi 59 wameondolewa kufanya kazi na wizara hiyo na majina yao kupelekwa bodi ya makandarasi wachukuliwa hatua.

"Tutashughulikia makandarasi wote wanaotaka kukwamisha upatikanaji wa maji, hatutacheka na mkandarasi na mhandishi wa maji, tutacheka kwa kuona maji yanapatikana," alisema.

Kuhusu malipo ya kufungiwa maji, alisema utaratibu umewekwa kuwa mwananchi aunganishiwe maji kisha alipe kwenye ankara yake ya maji kila mwezi.

Aweso alisema hivi karibuni atapokea ripoti ya bambikizi kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ripoti ya bili bambikizi.

Alisema mamlaka yoyote iliyotoa bili kinyume cha taratibu ya bei elekezi zitachukuliwa hatua kali za kisheria.

Kwa mujibu wa Aweso, wananchi wanatumia majisafi na salama vibaya kwa kuwa wanamwagilia maua wakati mvua inanyesha, kufyatulia matofali na wengine wakipiga mswaki, huku bomba lipo wazi maji yanamwagika.

"Tumeanzisha mfumo mpya wa bili kwa mamlaka za maji ili kudhibiti ubambikiwaji, kuhakikisha wasoma mita hawabambikii na kuhakikisha wanaposoma mita wanashirikisha wananchi," alisema.

Waziri huyo alipiga marufuku ukataji maji kipindi cha sikukuu na mwisho wa wiki, na kwa watakaofanya hivyo watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Aweso alisema ameshafanya ziara na kuona upotevu wa maji ni asilimia 46 na kugundua kuna wizi mkubwa wa maji, huku akitolea mfano wa Morogoro walikuwa wanaiba maji kwa zaidi ya Sh. milioni 100 na baadhi ya watumishi wanahusika.

"Mwananchi anatoa taarifa kwa mamlaka maji yanapovuja hawafuatilii, ila mwananchi huyo huyo akimtumia waziri akawatumia haraka wanachukua hatua na kupiga picha, tunataka nguvu wanayoitumia kufuatilia wanapoagizwa na viongozi hiyo hiyo waitumie wanapotumiwa taarifa na wananchi," alisema.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alisema serikali itatoa maji mto Ruvuma kuhudumia mikoa ya Kusini, mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwa ajili ya mkoa wa Simiyu.

# Waliosamehewa na Rais wauawa

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

WATU wawili wameuawa na wananchi wenye hasira wakituhumiwa kuhusika katika tukio la wizi huko Kwamatiasi wilayani Kibaha mkoani Pwani.

Kwa mujibu wa Jeshi la Polisi, watu hao ambao hivi karibuni walitoka jela kwa msamaha wa Rais, ni Ramadhani Mohamed (28), mkazi wa Kwamatiasi na Idd Hamis (30), mkazi wa Jamaika wilayani Kibaha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema jana kuwa awali watuhumiwa hao walifungwa kwa makosa ya wizi katika kesi ya jinai Na. 273/2020 na 260/2020 na walipata msamaha wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Aprili mwaka huu katika Gereza la Mkuza, Kibaha.

Kamanda alisema watuhumiwa hao walipoteza maisha wakiwa njiani kuwahishwa hospitalini kwa ajili ya kupata matibabu baada ya kuchukuliwa polisi kutoka mikononi kwa wananchi waliowapiga kwa mawe, mapanga na fimbo.

Kamanda Wankyo alitoa onyo kwa wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi.

Katika tukio lingine watu 21, wakiwamo wanawake watatu, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuhusika na matukio mbalimbali ya kukutwa na vitu mbalimbali vinavyodaiwa kuwa ni vya wizi.

Wankyo alisema watuhumiwa hao walikamatwa kwenye msako uliofanyika kwa kipindi cha wiki moja katika wilaya tano za kipolisi kwa lengo la kudhibiti na kuzuia makosa ya jinai na ya usalama barabarani.

Alisema watuhumiwa wanawake wanadaiwa kukutwa wakiuza uji pamoja na kete za bangi ambazo wamekuwa wakizificha kwenye biashara zao na pombe ya moshi.

Wankyo alisema watuhumiwa hao 21 ni pamoja na waliokamatwa kwenye tukio la kujichukulia sheria mkononi na kuwapiga na kuwasababishia umauti watu wawili wanaodaiwa kuhusika katika tukio la wizi huko Kwamatiasi, Kibaha.

Vitu walivyokutwa navyo watuhumiwa hao ni pamoja na bangi kete 89, sawa na gramu 44.5, pombe ya moshi (gongo) lita 23, televisheni nne, simu za mkononi tatu, kompyuta mpakato mbili, redio aina ya Kenwood, deki tatu, sabufa tatu na redio za gari mbili.

Vingine ni pasi ya umeme, mtungi wa gesi, ng'ombe wawili, pikipiki nne, mabati 29, vifaa vya kutengeneza vigae, ving'amuzi vitatu na jiko la gesi moja.

Kamanda Wankyo aliwaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kuwakamata watu wanaohusika na matukio ya uhalifu.


UNHCR
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**ADDENDUM TENDER NOTICE – EXTENSION OF DEADLINE SUBMISSION**

**INVITATION TO BID (ITB)
ESTABLISHMENT OF LOCAL FRAME AGREEMENTS FOR SUPPLY OF VARIOUS ITEMS**

**1. Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam had initially advertised in various newspapers the invitation of reputable and qualified suppliers to submit firm offers for the establishment of multiple Frame Agreements for the supply of any or all the below-listed Items.

**2. Requirements:**

| TENDER REFERENCE NUMBER | TENDER ITEM DESCRIPTION |
|---|---|
| ITB/2021/SUP/003 | Supply of Assorted Spare Parts |
| ITB/2021/SUP/005 | Supply of Tires |
| ITB/2021/SUP/007 | Supply of Uniforms and Shoes |

**3. Extension of deadline for submission**

Due to the upcoming Eid-El-Fitr holidays, the tenders above which were to be initially submitted by 14th May 2021, the deadline has now been extended to Tuesday **18th May 2021 at 1600 hours.**

# Kilio ukosefu maji chatawala bungeni

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

UKOSEFU, upotevu wa maji na madeni ya makandarasi jana vilitawala mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji, wabunge wakitaka hatua zichukuliwe haraka kuongeza kasi ya upatikanaji wa maji nchini ili kuwaondolea kero wananchi.

Watunga sheria hao walitaka gharama za kuunganishiwa maji kukatwa kwenye ankra na wananchi kuruhusiwa kununua vifaa kuliko utaratibu wa sasa wa kulazimishwa kununua kwenye mamlaka za maji.

Pia walisema kiwango cha upatikanaji wa maji kinachotajwa na wataalamu kuwa ni zaidi ya asilimia 86 kwa mijini na asilimia 72.3 vijijini, hakiakisi kiasi hicho na inawezekana kuwa ni chini ya asilimia 50.

Mbunge wa Viti Maalum, Esther Bulaya (CHADEMA), alisema upotevu wa maji ni tatizo sugu tangu mwaka 2010 na kwamba kati ya mamlaka za maji 23, mamlaka 21 zina upotevu wa maji kupita kiasi.

Kwa mujibu wa Bulaya, mwaka 2018/19 serikali ilipata hasara ya Sh. bilioni 77 na mwaka 2019/20 Sh. bilioni 155 na kwamba kwa miaka miwili zilipotea Sh. bilioni 332 ambazo zingechimba visima au kugharamia miradi mingi kwenye majimbo na kumtua mama ndoo.

"Tunajua kuna upotevu baada ya kukokotoa yanayozalishwa, miundombinu ya maji ni chakavu, ni muhimu kuziba mianya ya maji kupotea.

"Kanuni ya usambazaji wa maji serikali inapaswa kupeleka ruzuku kwenye mamlaka za daraja A hadi C na mwaka huu serikali imeshindwa kupekela fedha kwenye mamlaka 10, tunashindwa kutengeneza, huku hatupeleki fedha na tunataka kumtua mama ndoo?" Alihoji.

Kuhusu madeni ya maji, mbunge huyo alisema kuna Sh. bilioni 148 ziko nje huku serikali ikidaiwa Sh. bilioni 64, na Sh. bilioni 83 ni madeni ya viwanda na wateja wa kawaida.

"Serikali kutolipa makandarasi kwa wakati na kufanya riba kuongezeka ni tatizo lingine kubwa sana, mfano mradi wa Ruvu Chini riba imefikia Sh. bilioni 3.9, zingelipwa kwa wakati zingekamilisha miradi mingine kweye maeneo ya Moshi, Arusha na Dar es Salaam," alisema.

Alisema taarifa za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) zilionyesha upatikanaji wa maji katika baadhi ya maeneo Mkoa wa Pwani ni asilimia 96, lakini Mdhibiti na Mkakuzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alivyopita alibaini nia asilimia 53 na huenda ikashuka zaidi na kuwa asilimia 50," alisema. Aliitaka serikali kukamilisha mradi wa muda mrefu wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda kata 14 za Mji wa Bunda.

Mbung wa Viti Maalum, Esther Matiko (CHADEMA), alisema Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa ulijiwekea malengo ya kufia mahitaji kwa asilimia 85 vijijini na 90 mjini, huku miradi 1,423 ilitekelezwa na visima zaidi ya 100,00 na kwamba nusu yake havitoi maji.

Kuhusu mradi wa miji 28 wa zaidi ya Dola za Marekani milioni 460, alisema kuna taarifa kuwa idadi itapunguzwa huku umbali na mtandao wa maji ukiwa ni uleule, akitaka uchunguzi kufanyika juu ya mabadiliko hayo.

"Tunaomba sana ufanyike uchunguzi tena kupitia Kamati ya Maji, waunde tume kupitia huu mradi, ili tuende na utaratibu wa mwanzo na siyo ya sasa kupunguza miji, na ikiwezekana ipate maji, mtandao wa maji umepungua sana kama ilikuwa kata nane, zitaingia kata mbili.

"Kuna ubadhirifu wa fedha, bila kung'oa mizizi bado upatikanaji wa maji utakuwa ni historia katika maeneo mengi, tunaomba uwajibikaji kwa ambao wamehusika kwa upotevu wa fedha za miradi ambayo inahuishwa tena na kutumia mamilioni ya fedha," alisisitiza.

Mbunge wa Chemba, Mohamen Moni (CCM), alisema wilayani kwake wanaopata maji hawafiki asilimia 42 na kwamba kuna miradi iliyoshindikana.

Mbunge wa Nkasi Kusini, Vicent Mbogo (CCM), alisema katika jimbo hilo kuna kata tatu hazijawahi kupata mradi wowote wa maji na kwamba gari lake limegeuka gari la wagonjwa kubeba wananchi waliojeruhiwa na mamba wakati wanakwenda kutafuta maji.

"Wabunge wanasema wana miundombinu chakavu, kwangu haipo kabisa, wanasema kuna wanaokunywa maji ya njano kwangu ni tope, kuna mabomba ya maji yaliletwa yamekaa kwa zaidi ya miaka minane. Waziri ninaomba upimwe kwa kuleta maji Nkasi," alisema.

Mbunge wa Makambako, Deo Sanga, alisema wakandarasi katika jimbo lake wanadai serikali jambo lililosababisha miradi mingi kukwama na kutaka hatua kuchukuliwa ili wananchi wapate maji.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Emmanuel Tutuba, akisalimiana na Mwenyekiti Mwenza wa Mkutano wa Majadiliano ya Kimkakati kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo nchini, Zlatan Milisic, alipowasili kufungua mkutano huo uliofanyika katika ukumbi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia aeleza fursa za uwekezaji kwa mabalozi

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao nchini, kutumia fursa za uwekezaji zilizopo kwenye sekta ya kilimo, viwanda, utalii, ufugaji pamoja na uvuvi.

Amesema nchi hizo ziwe tayari kuwaleta wawekezaji kutoka nchi zao, kuja kushirikiana na Tanzania katika kuzitumia fursa hizo kiuchumi.

Rais Samia aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akipokea hati za utambulisho za mabalozi watano walioteuliwa kwa ajili ya kuziwakilisha nchi zao nchini.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, ilisema mabalozi hao ni Lebbius Tobias wa Namibia, Mary O'Nell (Ireland), Dk. Mehmet Güllüoglu (Uturuki), Marco Lombardi (Italia) na Ricardo Mtumbuida (Msumbiji).

Rais Samia baada ya kupokea hati hizo, aliwakaribisha mabalozi na kuwahakikishia kwamba Tanzania ipo tayari kushirikiana katika kuimarisha, kukuza zaidi uhusiano hasa kwenye masuala ya uchumi na ustawi wa jamii kwa manufaa ya pande mbili.

Pia Rais aliwataka mabalozi hao kufikisha salamu zake za shukrani kwa marais wa nchi wanazoziwakilisha na kuwahakikishia ushirikiano. Aidha, mabalozi hao walimshukuru Rais Samia kwa kupokea hati zao za utambulisho na kuwa tayari kukuza zaidi uhusiano kuahidi kutoa ushirikiano wa kutosha kufanikisha matarajio yaliyopo hasa kwenye kiuchumi.

Rais Samia ni mara ya kwanza kupokea hati za utambulisho za mabalozi, tangu aingie madarakani Machi, 19, mwaka huu.

# Wawekezaji zaidi waja kumaliza uhaba sukari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetoa ardhi kwa wawekezaji 14 katika mikoa minne, ikiwamo wawili watakaojenga viwanda vya sukari Morogoro na Kigoma ili kukabiliana na tatizo la sukari.

Hata hivyo, imetoa angalizo kwa wawekezaji hao kuhakikisha wanaendeleza ardhi waliyopewa vinginevyo watanyang'anywa.

Akikabidhi hati za ardhi ambazo zimesainiwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema Rais Samia alipoingia madarakani wiki ya kwanza ametoa idhini ya kuridhia uwekezaji huo na kiwanda cha Muhogo Kilwa.

"Serikali imetoa ardhi kwa wawekezaji 14, miongoni wawekezaji hao wapo wawekezaji wa kimkakati kuna wawekezaji wametaka 'industrial park' ambapo watawekeza viwanda zaidi ya 70, hili ni jambo kubwa," alisema.

Alisema uwekezaji huo utasaidia kutoa ajira kwa Watanzania ambapo wawekezaji hao watawekeza mikoa ya Pwani, Kigoma, Lindi na Morogoro.

"Kuna tatizo la uhaba wa viwanda vya sukari nchini, ambapo sekta binafsi imeingiza viwanda viwili vya sukari kwa mpigo ambapo kimoja kitakuwa Kigoma, wamepewa hekta 37,000 na zingine 10,000 zinashughulikiwa, ambaye anamiliki kiwanda cha karatasi Mufindi," alisema.

"Tunataka kutibu tatizo la upungufu wa sukari, lakini kiwanda cha sukari Morogoro, wamefanikiwa kwenye viwanda vingine leo tumewapa hekta 4,000, lakini kwa sababu kuna matumaini pale Mbigiri na kwingine, hawa wanatengeneza shamba lao la hekta 4,000 na kuweka kiwanda na wanategemea kununua miwa," alisema.

Alibainisha tatizo la Morogoro watu wamelima miwa mingi, lakini viwanda vya kuchakata miwa ni vichache, hivyo ujenzi wa kiwanda hicho utasaidia kupunguza tatizo la upungufu wa uzalishaji sukari ndani ya nchi.

"Kule Kilwa anaenda kulima mwenyewe sababu alikosa muhogo wa kununua ameona aanze mwenyewe kulima, na ataweka kiwanda kwanza cha kuchakata mihogo," alisema.

Kadhalika, Lukuvi alisema hakuna mwekezaji ambaye atapewa ardhi halafu akope fedha kwa kuweka rehani ardhi hiyo ili kuendeleza mradi mwingine na kwamba sheria imebadilishwa.

"Mtu yeyote atakayetumia hati hii kwenda kukopa fedha lazima benki hawatampa maana lazima fedha hiyo iendeleze ardhi hiyo hiyo uliyokopea, tofauti na zamani, benki itakayowapa mkopo kwa dhamana ya mashamba haya tupu halafu ukaenda kujenga apartment eneo jingine ukashindwa kulipa, itakula hasara maana sisi tutakunyang'anya," alisema.

Aliongeza "Wale wenzangu wa Dar es Salaam nawapa meseji Pugu Road Kamishna nilishaagiza naagiza tena, Pugu Road ilikuwa Industry area tulitoa vile viwanja kwa ajili ya viwanda, nataka mkafanye upekuzi wale wote waliokiuka sijui wamejenga vitu gani lazima warudi kwenye msingi."

"Hatuwezi kuwapa. Leo wanasema wanaenda kujenga 'industry park' tuje kuona wamejenga miti hatuwezi kukubali, sisi tunampa eneo akatengeneze kiwanda kama alivyosema.

# NSSF yapania kulipa wanachama kwa wakati

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, amemhakikishia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, kuwa katika mpango na bajeti ya mfuko ya mwaka ujao wa fedha 2021/2022, wamejikita zaidi katika vipaumbele saba vinavyoondoa kero za wanachama.

Mshomba alisema hayo mwishoni mwa wiki, wakati wa uzinduzi wa Baraza jipya la 47 la Wafanyakazi wa NSSF lililofanyika mkoani Morogoro.

Alitaja vipaumbele hivyo kuwa ni kuhakikisha wanaandikisha wanachama katika sekta binafsi na sekta isiyo rasmi na uboreshaji wa huduma ili kuondoa malalamiko.

"Tutahakikisha mifumo yetu (NSSF) iko vizuri na inakidhi matarajio yetu, katika hili tutatumia TEHAMA kazi zetu ziende vizuri na huduma kwa wateja zinatolewa," alisema. Vipaumbele vingine alivyovitaja ni mafunzo kwa wafanyakazi ili waweze kuelewa taratibu za mfuko,

mafunzo kwa wafanyakazi watoa huduma kwa wanachama ili waweze kuvaa viatu vya wanachama kwa kuzingatia maadili na kujenga timu moja na kuwafanya wafanyakazi kuwa sehemu ya mfuko huo.

Pia kuweka mazingira bora ya kazi na usimamizi madhubuti hasa kwa Menejimenti na Bodi ili waweze kufanikiwa katika malengo yao.

Akizindua Baraza hilo la Wafanyakazi wa NSSF, Waziri Jenista aliiagiza Menejimenti ya NSSF kuweka mifumo sahihi itakayoondoa changamoto za wanachama na wadau.

"Nawaomba mkatathmini mifumo iliyopo na ikiwezekana mtengeneze mifumo ambayo itamwezesha mwanachama kulipwa mafao yake bila kwenda kupiga magoti kwa wafanyakazi wa NSSF," alisema.

Aliwataka watumishi kuendeleza kasi ya kukusanya michango ya wanachama kwenye maeneo yote ya ajira ili inapotokea mfanyakazi amepata janga lolote, mfuko uweze kumlipa kwa wakati na bila ya usumbufu.

Naye Mwakilishi kutoka Chama cha Wafanyakazi wa Viwandani, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) na Mkuu wa Sekta za Taasisi za Fedha, Willy Kibona, alisema maelekezo yaliyotolewa na Waziri Jenista yamekuwa ni funzo kwa baraza hilo jipya pamoja na watumishi wote wa mfuko na kuahidi kuyatekeleza na kuyazingatia kama alivyoelekeza.

"Tunasema asante sana wa kutujengea misingi imara ya kuanza tena awamu ya miaka mitatu ijayo ya Baraza hili hususani katika kutuasa yale yote ambayo tunatakiwa kuyatekeleza kwa mujibu wa sheria ya NSSF," alisema.



Ujenzi wa daraja la waenda kwa miguu la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam, ukiwa umefikia hatua ya mwisho, daraja hilo litakuwa msaada kwa abiria na watu wengine wanaokwenda na kutoka katika stendi ya mabasi ya mikoani iliopo eneo hilo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Baraza lalaani mauaji ya mzee

**Na Marco Maduhu, KAHAMA**

BARAZA la Wazee Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, limelaani tukio la mauaji ya Mayombo Songo (75), mkazi wa Wendele katika manispaa hiyo, anayedaiwa kuuawa kwa kukatwa mapanga na watu wasiojulikana.

Wazee walipaza kilio hicho kwenye kikao cha kuthamini na kupanga mikakati ya kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wazee kwenye manispaa hiyo kilichoandaliwa na Shirika la Tawlae linalotekeleza miradi ya kutetea haki za wazee mkoani Shinyanga.

Katibu wa baraza hilo, Underson Lyimo, alisema mauaji ya wazee yalikuwa yamekwisha, lakini mwaka huu yameanza kuibuka upya, hivyo kuitaka serikali na vyombo vya usalama kuyadhibiti.

"Baraza la Wazee Manispaa ya Kahama tunalaani mauaji ya huyu mzee mwenzetu ambaye aliuawa kwa kukatwa mapanga usiku akiwa amelala nyumbani kwake na watu wasiojulikana, tunaitaka serikali na vyombo vya usalama kuyadhibiti matukio haya ili yasitokee tena," alisema Lyimo.

Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi wilayani Kahama, Elias Sikanda, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Polisi wilayani humo, alithibitisha kutokea kwa mauaji ya mzee huyo, na kubainisha kuwa bado wanawasaka watu waliohusika na mauaji hayo.

Pia alisema Jeshi la Polisi limejipanga vyema kidhibiti mauaji ya wazee yasitokee tena, wakitumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na mikutano ya hadhara kutoa elimu kwa wananchi juu ya kuthamini wazee na kuacha kutekeleza mauaji dhidi yao.

Ofisa Miradi wa Tawlae, Winie Hinaya, alisema jamii inapaswa kuwalinda wazee na kuwatunza, badala ya kuwaona kama mikosi kwao huku wakiwatuhumu kwa ushirikina.

# Operesheni wapita barabara za DART yaanza

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, wameanza operesheni maalum ya kukamata wanaopita kwenye barabara za Mabasi Yaendayo Haraka, wakiwamo waendesha bodaboda, bajaji, magari binafsi ya serikali na ya majeshi.

Akizungumza katika eneo la operesheni hiyo Kinondoni Mwanamboka, mkoani Dar es Salaam, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Dumu Mwalugenge, kutoka Makao Makuu ya Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, alisema operesheni hiyo ni endelevu na inalenga kukomesha vitendo vya uvunjifu wa sheria vinavyofanywa na baadhi ya wananchi wasiotaka kutii sheria bila shuruti.

"Unaona baadhi ya madereva wa pikipiki wakiwa wamekamatwa, hii ni kuonyesha msisitizo kwamba lazima sheria zifuatwe na kusiwe na ulazima wa kutumia nguvu mara kwa mara, kwani jamii iliyostaarabika inafuata sheria kanuni na taratibu zilizowekwa ili kuzuia ajali za mara kwa mara kwenye barabara za mabasi yaendayo haraka," alisema.

Mwalugenge alisema barabara hizo zimejengwa mahsusi kwa ajili ya mabasi ndio maana michoro yake chini kwenye sakafu za barabara imeandikwa 'Bus' pekee kwa ajili ya mabasi na sio bodaboda, bajaji wala magari binafsi na hata ya serikali.

Alisema madereva wa magari ya serikali ndio wanaongoza kwa kuvunja sheria hasa kupitisha magari kwenye barabara za mabasi yaendayo haraka na kuwaonya wenye tabia hiyo kuacha mara moja kwa kuwa sheria haiangalii kazi wala cheo cha mtu yeyote atakayekiuka atashughulikiwa.

"Madereva wa serikali hawako juu ya sheria natoa onyo waendelee kutii sheria bila shuruti ndio maana unaona operesheni hii inayoambatana na kutoa elimu ya matumizi sahihi ya barabara za mabasi yaendayo haraka inaendelea," alisema.

Pia katika operesheni hiyo DART kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wanatoa elimu ya matumizi sahihi ya barabara hizo ili kusaidia kupunguza ajali za mara kwa mara zinazosababishwa na matumizi yasiyofaa ya miundombinu hiyo.

Miongoni mwa matumizi yasiyofaa ya barabara hizo ni pamoja na kupitisha magari binafsi na ya serikali, pikipiki pamoja na bajaji, kuvuka maeneo ambayo hayana vivuko vya waenda kwa miguu na vyombo vingine vya moto pamoja na vyombo baridi kama baiskeli na maguta kuvuka kwenye vivuko vya waenda kwa miguu wakiwa waendesha badala ya kuvikokota.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Yaibuliwe mazao zaidi kumaliza uhaba mafuta

KATIKA moja ya mambo ambayo yameumiza vichwa vya Watanzania, ni pamoja na uhaba na ughali wa mafuta ya kula, ambao umesababisha walazimike kuyatafuta kwa gharama kubwa lakini wakati mwingine bila mafanikio.

Ukosefu wa mafuta uliibuka miezi kadhaa sasa na hadi sasa unaendelea na hata kama yapo yaliyokuwa yamefichwa kwenye maghala yanapopatikana yanauzwa kwa bei ambayo ni kero kwa watumiaji.

Pamoja na hayo kuna mafuta yasiyofahamika ubora ambayo yanauzwa kwenye maduka mitaani, mengine hayeyuka, kuna yanayofanana na masimbi na hata yenye rangi ambazo hazifahamiki lakini kwa vile kuna uhaba wa mafuta, imekuwa ni fursa hata wale waliokuwa wanaogopa kuyauza kwa hofu ya kuwa na dosari, sasa wameyaingiza sokoni.

Ni habari njema serikali inapotangaza kuwa imekuja na mwarobaini wa uhaba wa mafuta hayo na kwa sasa inafanya mchakato wa muda mfupi kukabiliana na tatizo la uhaba wa bidhaa hiyo muhimu.

Inazitaja sababu za kuadimika kuwa ni kutokana na viwanda vya mafuta nchini kufungwa kwa sababu ya kodi ya mafuta ghafi kuwa juu, hivyo matarajio ya muda mfupi ndani ya miezi miwili ijayo ni kuanza kuvuna alizeti na kwamba bei ya mafuta itashuka kwa vile itaanza kusindikwa viwandani.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Profesa Kitila Mkumbo, ananukuliwa akisema, kuwa kwa sasa wafanyabiashara wanalazimika kuagiza mafuta ya mawese yaliyochakatwa kutoka nje na gharama yake alipandishwa mara mbili.

Anasema kuagiza mafuta hayo kutoka nje kunatokana na viwanda vya hapa nchini vilivyokuwa vinachakata mafuta kufungwa vyote vitatu kwa sababu alizosema ni kufanya kazi kwa 'ujanjaujanja' mwingi.

Anasena wawekezaji walisema walikuwa wanachakata mafuta kutoka ndani ya nchi wakati walichokuwa wanafanya ni kuyaagiza kutoka nje ya Tanzania na kuongeza kuwa amewaagiza kuandaa hoja ili ziwasilishwe kwenye mchakato wa kuangalia suala la mafuta ikiwamo kubadilisha gharama za kodi wanazolalamikia kutoka asilimia 25 kurudi asilimia sifuri kama ilivyo kwa nchi za Afrika Mashariki.

Ni vyema sasa kila upande kutimiza wajibu wake kwa kuzingatia mapendekezo ya serikali ili kumaliza uhaba wa mafuta na hivyo kuwawezesha wananchi kupata huduma hiyo bila usumbufu kama huo ambao umejitokeza sasa.

Tunasema hivyo kwa sababu tatizo la uhaba wa mafuta halijaanza leo. Taarifa kuwa Tanzania iliipa Malaysia utaalamu na mbegu za michikichi na sasa inanunua mafuta ghafi kutoka kwake hazijaanza leo. Ni wakati wa kuona matatizo kama hayo yanatatuliwa kwa kuwa kuna mbegu nyingi zinazoweza kuzalisha mafuta kuanzia karanga, korosho, michikichi, alizeti hadi mbegu za pamba.

Tunashauri Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) isaidie kufanikisha kupatikana mbegu za mimea inayozalisha mafuta ili kuzalishwa kwa wingi na kuwa na uhakika wa mafuta yanayotoka nchini kwa usalama wa walaji na pia kuinua uchumi wa wakulima wetu.


Inashangaza kusikia malalamiko ya uhaba wa mafuta ya kula pamoja na sukari kila mwaka ndiyo maana tunaishauri serikali iweke mikakati ya kumaliza tatizo hilo, lakini ni vyema wafanyabiashara wanaotuhumiwa kufanya 'ujanjaujanja', waachane na mtindo huo unaowaumiza wananchi.

Kila upande ukitimiza wajibu wake tunaamini kwamba kero zinazotokana na uhaba wa mafuta ya kula zitakuwa zimepatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Lakini, utafiti zaidi ufanyike kupata mafuta kutoka vyanzo vingine badala ya kutegemea mimea ya mafuta ikiwamo alizeti, michikichi na karanga. Mazao kama nazi, ubuyu na hata maparachichi pia yafanyiwe uchunguzi kumaliza uhaba.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mwanafunzi wa leo anakumbushwa kujiandalia ratiba nyumbani, shuleni

Na Sabato Kasika

KUTENGA muda wa kujisomea ni miongoni mwa njia zinazoweza kumsaidia mwanafunzi kujiandaa na kufanya vizuri katika masomo na mitihani yake bila kujali anasoma katika kiwango gani.

Ili kufanikisha hilo, ratiba hiyo inatakiwa kuandaa utaratibu na mikakati ya kujisomea kuanzia nyumbani hadi shuleni na hata wakati wa mapumziko na likizo za mihula.

Kimsingi, ratiba ina nafasi kubwa ya kumsaidia mwanafunzi kufikia malengo yake ya kufaulu, hivyo ni vyema aipange ili kujisomea huku akifuata ratiba yake ya darasani.

Kwa ujumla kupanga ratiba ni muhimu na ni utaratibu unaotakiwa kufuatwa na mwanafunzi, wazazi na walezi ili waweze kuitekeleza inavyotakiwa, kwa lengo la kumsaidia kutimiza malengo yake.

Iwapo kila mwanafunzi atajiwekea ratiba ya kujisomea nyumbani huku wazazi nao hawapi kazi nyingi au majukumu mengine, itakuwa rahisi kufanya vizuri darasani, kwa kuwa atakuwa ameshafanya mapitio mengi.

Kwa kujali umuhimu huo wa kutenga muda wa kujisomea, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, anawaomba wazazi na walezi kuwapunguzia kazi watoto wao wanaojiandaa na mitihani ili waweze kujisomea.

Mtaka anatoa rai kwa wazazi na walezi wenye watoto walio katika madarasa ya mitihani ya taifa kuwapunguzia kazi ili wanafunzi hao waweze kupata muda wa kujiandaa na akizungumza wiki iliyopita mjini Bariadi wakati wa futari maalum iliyoandaliwa na ofisi yake kwa ajili ya Waislamu waliofunga Ramadhani.

Matarajio ya mkuu huyo wa mkoa ni kuhakikisha Simiyu inabaki kuwa miongoni mwa mikoa mitano inayofanya vizuri katika elimu nchini, huku malengo ya mwaka huu ikiwa ni kuona wanatoka kwenye nafasi ya tano.

Wanatamani kuwa nafasi ya tatu na kufikia nafasi ya kwanza, hivyo anawaomba wazazi na walezi wote wa mkoa wa Simiyu wenye watoto wa madarasa ya mitihani wawapunguzie kazi ili wapate muda wa kujisomea na kufanya matayarisho ya mitihani yao ya taifa.

Anawataka wazazi kutowaruhusu wanafunzi kwenda katika minada kufanya biashara badala yake wahakikishe wanafunzi wote wanahudhuria masomo, ili kuendelea kuinua mkoa huo kielimu.

Kinachofanywa na mkoa huo, ni mfano wa kuigwa ili kusaidia kuongeza ufaulu, hasa kwa kutambua kuwa si rahisi mwanafunzi kufanya vizuri darasani au katika mitihani bila kupata muda wa kutosha wa kujisomea.

Wanafunzi wanawajibu wa kusaidia kufanya shughuli za nyumbani, lakini shughuli hizo zisiwabane hadi wakose nafasi ya kujisomea, bali wapunguziwe kazi ili iwe rahisi kuwa na ratiba ya kujisomea.

**Anawataka wazazi kutowaruhusu wanafunzi kwenda katika minada kufanya biashara badala yake wahakikishe wanafunzi wote wanahudhuria masomo, ili kuendelea kuinua mkoa huo kielimu.**

Suala hilo liko ndani ya uwezo wa wazazi na walezi na ndiyo maana mkuu wa mkoa amewaomba kuzingatia hilo, hasa kwa kuzingatia kwamba mitihani ya taifa iko karibu kuanza kufanyika, hasa kwa wanafunzi wa darasa la saba.

Lakini, pamoja na hayo kuwa na ratiba ya kujisomea isiwe kwa wanafunzi wanaojiandaa kufanya mitihani tu bali uwe ni utaratibu wa kawaida kwa lengo la kuwajengea uelewa zaidi wa masomo mbalimbali.

Njia hiyo pia inamwezesha mwanafunzi kuwa na uwezo wa kuuliza maswali mbalimbali yanayohusu mada zilizopita pale mwalimu akifika darasani wakati akikumbushia yale yaliyofundishwa kwenye vipindi vilivyotangulia au iwapo akiuliza kuna mtu hakuelewa somo lililopita mwenye ratiba na anayeifuatilia anapata nafasi ya kuuliza aliyoyabaini.

Hivyo, mwanafunzi kuwa na ratiba ya kujisomea nyumbani ni muhimu, lakini itakuwa matokeo mazuri kama ataheshimiwa na wote kuanzia wazazi na walezi pamoja na mhusika.

Ikumbukwe yote hayo yatafanikiwa kama walezi na wazazi wataacha kumpa majukumu mengi yanayomkosesha muda wa kujisomea.

HABARI KITAIFA

# Mbunge alia na ahadi za marais

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

MBUNGE wa Njombe Mjini (CCM), Deodatus Mwanyika, ameikumbusha serikali kutekeleza ahadi ya upatikanaji wa maji katika jimbo lake zilizotolewa kwa nyakati tofauti na viongozi wakuu wa nchi, Rais Samia Suluhu Hassan na Hayati Rais John Magufuli.

Amesema kuwa kwa nyakati tofauti viongozi hao, akiwa Rais Samia, akiwa mgombea mwenza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Hayati Magufuli akiwa mgombea urais miaka 2015 na 2020, walipita katika jimbo hilo na kuahidi kutatua tatizo la ukosefu wa maji.

Mwanyika amesema kuwa tangu kipindi hicho hadi sasa, maeneo mengi katika jimbo hilo bado yanakabiliwa na ukosefu wa majisafi na salama.

"Hayati Rais Magufuli kwenye kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2015 alipopita Njombe aliwauliza wananchi 'shida yenu nini?', wakamjibu kuwa ni maji.

"Hata mwaka 2020 alipopita tena na kuwauliza, wakajibu maji. Hata Rais Samia alipokuwa mgombea mwenza kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 alisimamishwa na wananchi wa Njombe na kumwelezea shida ya maji naye akaahidi kutatua," alisema Mwanyika bungeni juzi.

Mwanyika alisema kuwa aliyekuwa Waziri wa Maji kipindi hicho, Makame Mbarawa, aliahidi ndani ya miaka miwili shida ya upatikanaji wa maji mkoani Njombe ingetatuliwa.

Aliongeza kuwa Mji wa Njombe una kata 13. Kati yake, 10 zipo vijijini na kata tatu zipo mijini, lakini kata zote za mjini hazina maji.

"Tunapata wasiwasi na huo mradi wa miji 28 kama tutapata maji, kwa sababu awali Njombe tulikuwamo katika mradi wa miji 16 lakini hatukupata maji.

"Nikuombe waziri nenda katekeleze ahadi za viongozi wakuu wa nchi walizozitoa," alisema Mwanyika.


Alisema mikoa yote mipya iliyoanzishwa imekumbukwa kupatiwa miradi ya maji lakini Mkoa wa Njombe umesahaulika.

"Kuna mradi wa Igogwi ambao umetengewa fedha kidogo Sh. bilioni nne, hadi leo haujakamilika, ninaamini kumesababishwa na watendaji wazembe.

"Wataalamu waliambiwa kuwa mtambo mnaouweka kwa ajili ya usambazaji wa maji kwenye vijiji vinane hautoshi lakini hawakusikia, matokeo yake hadi leo wananchi hawana maji," alilalamika.

Alisema Mradi wa Mji wa Njombe eneo la Kibena, Kata ya Ramadhani umekuwa na mafanikio makubwa na wananchi wameanza kupata maji.

Alisema mradi huo umefanikisha upatikanaji wa maji katika Hospitali ya Wilaya, wananchi 3,000 wameunganishwa lakini bado kuna zaidi ya wananchi 3,500 hawajaunganishwa na huduma ya maji.



Kiongozi wa Wanafunzi wenye Ulemavu Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Kelvin Mkude, akisoma risala wakati wa kongamano la wenye ulemavu lililowakutanisha kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali yanayowahusu wanafunzi wenye ulemavu na maendeleo lililokuwa na kauli mbiu isemayo "Ulemavu si Kukosa Uwezo" ukumbi wa Chuo Kikuu cha Dodoma jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yaokoa zaidi ya mil. 600/-

**Na Ada Ouko, MUSOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Mara, imeokoa zaidi ya Sh. milioni 689.3 kilichodaiwa kutaka kuporwa kupitia malipo ya makandarasi na wazabuni waliokuwa wakitekeleza kazi za ujenzi wa miundombinu ya majengo na barabara mkoani hapa.

Akizungumza jana ofisini kwake na waandishi wa habari, Mkuu wa TAKUKURU mkoani Mara, Hassan Mossi, alisema ofisi yake katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Machi, mwaka huu, ilifanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 8.188 na kubaini kuwapo mianya ya rushwa.

"Tumeweza kudhibiti mianya ya rushwa na hatimaye kufanikiwa kuokoa kiasi hicho cha fedha (Sh. 689,317,212.00) ambacho kilikuwa kifanyiwe ubadhirifu kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007," alisema Mossi.

Vilevile, alisema katika kipindi cha Januari 2021 hadi Machi 2021, ofisi yake iliendelea kufuatilia malalamiko na tuhuma mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa miradi kadhaa ya maendeleo inayotekelezwa kwa kutumia makusanyo ya ndani ya Sh. 891, 288,244.

Pia ofisi hiyo ilifanya uchunguzi dhidi ya tuhuma za mkopeshaji mmoja anayedaiwa kumkopesha mama mmoja pesa ambaye kwa sasa ni marehemu na kuimiliki nyumba yake kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2207 Kifungu cha 23.

"Baada ya kusikia kuwa mama huyo amefariki mkopeshaji huyo alitengeneza nyaraka zinazoonesha walifanya mauziano ya nyumba hiyo toka mwaka 2001 na mpaka sasa mkopeshaji anaimiliki nyumba hiyo...ofisi yangu inakamilisha uchunguzi huo na hatimaye kulifikisha suala hilo mahakamani," alisema.

Madai mengine yaliyoshughulikiwa na ofisi hiyo katika kipindi hicho ni pamoja na kulirejeshea Kanisa la Mennonite Serengeti kiasi cha Sh. 3,000,000 zilizolipwa zaidi katika mazingira ya rushwa kutokana na mauzo ya gari.

Madai mengine ni ya mwalimu mstaafu aliyekopeshwa Sh. 1,400,000 na baada ya mafao yake kutoka mkopeshaji alichukua Sh. 66,000,000, lakini baada ya TAKUKURU kuingilia kati mkopeshaji huyo amekwisha mrejeshea mwalimu huyo Sh. 30,000,000.

# Waendeleza kilio uhuru wa habari

**Na Beatrice Shayo, MOROGORO**

KATIBU Mkuu wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, amesema bila kushughulikiwa kwa sheria kandamizi kwa vyombo vya habari ikiwamo kufungiwa kwa vyombo hivyo nchini itaendelea kuviathiri.

Mukajanga aliyasema hayo jana mkoani Morogoro katika mkutano wa siku tatu kwa ajili ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari wanaofanya kazi zao kwenye mitandao ulioandaliwa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC).

Alisema ni vizuri sheria za vyombo vya habari zinazolalamikiwa kuwa ni kandamizi na zinaminya uhuru wa habari zinapaswa kuondolewa.

"Aprili 6, mwaka huu Rais Samia Suluhu Hassan akiwa anawaapisha viongozi aliowateua aliongelea kidogo suala la vyombo vya habari na aliagiza vyombo vya habari vifunguliwe, sasa hili lilibaki kuwa mjadala, wengi tulisikia vyombo vya habari vifunguliwe na wasaidizi wake wakisema ni vyombo vya habari vya mtandaoni, hivyo kwa sababu ofisi ya Rais haijatoa kauli juu ya taarifa ya wasaidizi hao agizo la kufunguliwa vyombo vya habari ndio sahihi," alisema.

Aliongeza: "Tunadhani bila kushughulikia sheria zinazoongoza, zinazosimamia na kudhibiti kazi zetu, tatizo halitaweza kuondoka. Kwa nia njema anaweza akaja kiongozi akaamua kama hivyo mfungulieni mtu fulani ndani ya ile sheria bado ipo, maana yake kesho anaweza akapata tatizo mtu mwingine au yuleyule aliyefunguliwa akapata tatizo kutokana na sheria zile zile."

Alisema suala hilo linaonyesha umuhimu wa kutizama mazingira yao kwa undani zaidi kwa kuwa vyombo vya habari jukumu lake ni moja, nyenzo na utaratibu ndivyo vinatofautiana iwe kwenye gazeti, redio, mtandaoni na televisheni.

Alisema waandishi wa mitandao ni watu muhimu wanawafikia watu wengi zaidi na vizuri kuhakikisha wanafanya kazi zao kwa kuzingatia taaluma na kuepuka kuweka taarifa za uongo.

Naye Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, alisema mafunzo hayo ni kwa ajili ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari wa mtandaoni kuhakikisha habari wanazoziweka zinakuwa sahihi.

Alisema kutokana na maendeleo ya teknolojia watu wanapata habari kwa njia ya mtandao, hivyo ni muhimu kuweka habari zenye uweledi.

Alisema wakati mwingine wanaweka habari za umbea ama ambazo hazina uweledi na habari za kijamii zikiachwa kupewa kipaumbele.

Kaimu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile,

alisema, mchakato wa mabadiliko ya sheria za mtandaoni umeanza kufanyiwa kazi na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na kuwaomba wadau kujitokeza kutoa maoni yao.

# Kuteua wapinzani serikalini kwawaibua wazee CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Wazee wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAZECHA), limepongeza kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kupanga kuteua viongozi wa kufanya naye kazi bila kuangalia vyama vyao vya siasa wanavyotoka, lakini limempa ushauri.

Baraza hilo limemshauri sheria zifanyiwe marekebisho ili anayeteuliwa asilazimike kuhama chama chake.

Pia limemshauri Rais Samia kuangalia uwezekano wa mchakato wa kupata Katiba mpya kwa kuanza na rasimu iliyofanywa na tume ya Jaji na Waziri Mkuu Mstaafu, Jaji Joseph Warioba.

Limemshauri kufuta sheria zote mbovu na kupeleka sheria bungeni ambayo itatambua umoja wa kitaifa ili pale anapoteua viongozi kutoka vyama vingine vya siasa kusiwe na ulazima wa viongozi hao kubadili vyama vyao wanakotoka.

Jambo jingine ambalo walishauri ni kufanyika mchakato wa kupelekwa sheria ya wazee bungeni ambayo itatumika kuangalia changamoto mbalimbali zinazolihusu kundi hilo.

Akizungumza kwa niaba ya wazee hao wa chama hicho katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Makamu Mwenyekiti wa Baraza hilo, Suzan Lyimo, alisema yapo mengi ambayo Rais Samia amepanga kuyafanya, lakini ili kufanikiwa, ni lazima sheria zifanyiwe mabadiliko.

"Tulisikia kauli ya Rais Samia wakati akizungumza na wazee, kwamba katika kujenga uchumi, atateua mtu ambaye anaona anafaa kuendana na weledi wake na tabia zake isipokuwa kama ana matatizo ya usalama na kimaadili, sisi wazee tumelipokea suala hilo kwa mikono miwili kwa sababu hata Katiba inasema kila mtu ana haki ya kisheria ya kufanya kazi mahali popote na inakataza ubaguzi wa aina yoyote," alisema Lyimo.

"Na Rais Samia siyo wa kwanza ambaye atafanya hivyo kwa sababu tunafahamu pia hata Hayati John Magufuli alifanya hivyo kwa kuteua baadhi ya viongozi kutoka vyama vya upinzani, lakini tuliona ilibidi wahame vyama vyao."

"Kwa hiyo, pamoja na nia nzuri ya Rais Samia, sisi kama wazee wa CHADEMA tunamshauri, kwanza kama kweli ana nia ya dhati ya kuwateua wanaotoka kwenye vyama vya siasa vya upinzani kwa kuangalia weledi, tunahitaji kabla ya kuteua awasiliane nao au afanye mawasiliano na viongozi wa vyama husika."

"Na tunadhani kwamba zile nafasi ambazo ataona moja kwa moja zina mgongano wa masilahi kwa vyama husika, kwamba mteuliwa itabidi ahame chama, tunamwomba asizifanye, labda kama kutakuwapo na mabadiliko ya sheria. Kwa nchi zilizoendelea zinaangalia weledi kuliko itikadi za vyama, kwa sababu vinapita."

"Zanzibar kuna kitu kinaitwa umoja wa kitaifa, lakini kwa huku Bara hatuna utaratibu huo, kwa hiyo kama Rais Samia ana lengo la kuteua watu kutoka sehemu yoyote bila kuangalia chama, basi sheria ibadilishwe halafu baadaye Katiba iweke msingi wa kuwa na umoja wa kitaifa ili mtu anapoteuliwa asiwe na mgongano wa maslahi wa kusababishwa ahame chama chake hata kama anakipenda."

Pia lilimshauri Rais Samia kwamba endapo atapanga kuongeza mishahara kwa watumishi wa umma, nyongeza hiyo izingatie na miaka yote ambayo serikali haikuwaongezea.

"Tunamshauri Rais Samia kwamba nyongeza ya mishahara itakapokuja kupandishwa iwe kwa kuangalia na miaka yote ambayo mishahara hiyo haikuongezwa.

Pia walishauri serikali kuweka utaratibu wa kutenga fedha ambayo itatumika kwa ajili ya kuongeza mishahara ya watumishi kila mwaka.

"Rai yetu ni kwamba ni lazima kuwe na tegemeo kwa ajili ya kupandisha mishahara kwa watumishi kwa sababu majanga kama magonjwa ya corona hayaishi. Hawa watu ambao hawajapandishwa mishahara na madaraja kwa muda mrefu, itakapokuja kuongezwa maana yake itachukua na mapungufu ya miaka yote."

"Kuanzia mwaka ambao hawakupandishwa madaraja na mishahara hiyo kwa sababu bila hivyo kama kuna mfanyakazi alitakuwa kustaafu kwa Sh. milioni 50 atastaafu kwa Sh. milioni 40.



Mkuu wa Wilaya ya Korogwe Mkoa wa Tanga, Kissa Gwakisa, akipokea sehemu ya madawati 150 na mabati 170 kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro (kulia), katika hafla iliyofanyika Shule ya Msingi Kwakombo ukiwa ni utaratibu wa benki hiyo kurejesha sehemu ya faida kwa jamii, msaada huo una thamani ya Sh. milioni 15, kushoto ni Meneja wa NMB tawi la Korogwe, Lugano Mwampeta. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ongezeko la maji ziwani lahamisha mwalo, soko

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imesema inatafuta eneo kwa ajili ya kuweka mwalo na soko la muda la kuuzia samaki katika Kata ya Kasanga Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo anayeshughulikia Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alisema wameamua kufanya hivyo kufuatia mwalo na lililokuwa soko la kata hiyo kujaa maji baada ya kina cha maji cha Ziwa Tanganyika kuongezeka.

Dk. Tamatamah amesema hayo kutokana na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya soko na mwalo kufunikwa na maji na kubainisha kuwa wizara inatafuta eneo la muda huku ikitafakari pia mipango ya muda mrefu kujenga sehemu ambayo ni salama zaidi.

Akizungumzia athari iliyojitokeza kutokana na uharibifu wa miundombinu ya soko hilo, Dk. Tamatamah alisema lilikuwa na msaada mkubwa kwa wavuvi wakati wa mavuno kwa kuwa walikuwa hawawezi kuuza samaki wote kwa wakati mmoja, hivyo walikuwa wakiwahifadhi na kuwauza kwa bei nzuri.

Alisema kwa sasa hakuna sehemu maalum ya kushushia samaki, hivyo wavuvi wanashushia maeneo mbalimbali ambayo hayana ubora.

Dk. Tamatamah alisema uwapo wa eneo la awali la kuuza samaki Kasanga lilikuwa linaunganisha pia watu zaidi ya 1,000 kila siku wanaoendesha shughuli mbalimbali katika eneo hilo.

Ofisa Mfawidhi na Msimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Kanda Kuu ya Tanganyika, Juma Makongoro, alisema kuongezeka kwa kina cha maji katika ziwa kumeathiri pia ofisi yao.

Makongoro aliwataka wananchi wa eneo hilo kuuza samaki nchi jirani ya Zambia kwa kutumia utaratibu wa kuwashirikisha watu au makampuni yenye leseni za kusafirisha samaki kwenda nje ya nchi ili wafanye biashara hiyo kwa njia halali badala kuuza kinyemela.

Naye Ofisa Mifugo na Uvuvi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Wilbroad Kansapa, alisema kujaa kwa maji katika soko hilo la Kasanga na viwanda viwili vya kuchakata samaki katika eneo hilo kuna athari kubwa kwa uchumi wa wananchi na halmashauri kwa ujumla.

# Angalizo boti ikipelekwa Kikwajuni uchumi wa bluu

**Na Peter Haule, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Zanzibar, Haroun Ali Suleiman, amewataka watakaopewa jukumu la kuendesha boti iliyotolewa kwa Taasisi ya Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Jimbo la Kikwajuni kwa ajili ya shughuli za uchumi wa bluu kuwa waaminifu ili kutimiza lengo lililokusudiwa.

Waziri Suleimani alitoa rai hiyo kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wakati wa kukabidhi zawadi kwa washindi wa Shindano la Kuhifadhi Quran pamoja na kukabidhi boti kwa Taasisi ya Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Jimbo la Kikwajuni, yaliyoandaliwa na kutolewa na Naibu Waziri Fedha na Mipango na Mbunge wa jimbo hilo, Mhandisi Hamad Yussuf Masauni.

Alisema bila kuwa na uaminifu katika matumizi ya boti, hakutakuwa na tija ya boti hiyo, hivyo kudidimiza lengo la Taasisi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la kuwapatia ajira vijana kupitia boti itakayotumika katika shughuli za uvuvi.

"Nimewahi toa boti mbili, tatu kwa ajili ya uvuvi, lakini kila nikihitaji kupata mrejesho, naambiwa leo baharini hakuingiliki au samaki hawapatikani, wakati napata taarifa kwa wengine kuwa samaki wamepatikana, kama hakutakuwa na vijana waaminifu, basi mradi huo hautaendelea," alieleza Waziri Suleiman.

Kwa upande wake, Masauni, alisema kuwa serikali imekuwa ikiweka miundombinu wezeshi kwa wananchi, lakini kutokana na kukosekana kwa uaminifu, miundombinu huharibiwa na miradi kufa, hivyo ameamua kutoa boti kwa Taasisi Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Kikwajuni ambayo inasimamiwa na watu wenye imani ya dini ili kukomesha ubadhirifu na kuleta tija stahiki.

**"Nimewahi toa boti mbili, tatu kwa ajili ya uvuvi, lakini kila nikihitaji kupata mrejesho, naambiwa leo baharini hakuingiliki au samaki hawapatikani, wakati napata taarifa kwa wengine kuwa samaki wamepatikana, kama hakutakuwa na vijana waaminifu, basi mradi huo hautaendelea," alieleza Waziri Suleiman.**

# SADC yaja na mikakati ya uhakika wa chakula

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

IMEELEZWA kuwa takribani watu milioni 5 katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), hawana uhakika wa chakula na lishe.

Waziri wa Kilimo, Prof. Aldof Mkenda, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki baada ya mkutano wa pamoja wa Mawaziri wa Kilimo,Mifugo kutoka nchi za SADC wenye lengo la kujadili masuala ya uhakika na usalama wa chakula.

Prof. Mkenda alisema katika mkutano huo moja ya mambo ambayo wamekubaliana katika nchi hizo, ni kuhakikisha wanaboresha masuala ya kilimo ili kuondoa tatizo la kukosa uhakika wa chakula kwa watu.

Waziri huyo alibainisha mikakati waliojiwekea kuhakikisha wanaondoa tatizo hilo ni kila nchi inakuwa na uhifadhi wa vinasaba vya mimea ya asili, kuimarisha utafiti wa kilimo na chakula.

Pia, alisema taasisi zinazohusika kuhakikisha zinasimamia masuala hayo kwa kina.

"Tumekuwa na mkutano mzuri sana,Mawaziri wa nchi za SADC, tunahakikisha yale mambo ambayo tunayakubali Tanzania na nchi nyingine yanatekelezwa," alisema Prof. Mkenda.

Kadhalika, alisema wamezungumzia masuala ya kulima mazao ya mifugo na uvuvi ili kuhakikisha kwamba wanajenga uhakika wa chakula cha kutosha na kuweka lishe nzuri katika nchi za SADC.

Hata hivyo, alisema wanavyojenga mahusiano mbalimbali na nchi hizo ni moja ya sababu ya kutafuta masoko, kwa sababu katika nchi za SADC kuna nchi zenye uchumi mkubwa sana, mfano Afrika Kusini,Angola ikifuatiwa na Tanzania.

Aliwahamasisha Watanzania kutumia fursa ya masoko hayo ili kujiinua kiuchumi.




Meneja wa Afya kutoka Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Jerome Materu (wa pili kulia), akimkabidhi Meneja wa Kiwanda cha TBL Plc cha Dar es Salaam, Patel Kilovela, tuzo na cheti cha ushindi katika sekta ya viwanda wakati wa Wiki ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, hafla hiyo, ilifanyika mwishoni mwa wiki jijini Ilala. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Wanafunzi 10 washinda shindano la insha

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI 10 kati ya 214 kutoka vyuo 32 vya elimu ya juu na vya kati nchini, wameibuka washindi wa shindano la insha lililoandaliwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Viwango Afrika (ARSO) yaliyofanyika mwishoni mwa wiki.

Maadhimisho ya Siku ya Viwango Barani Afrika hufanyika kwa lengo la kuamsha uelewa miongoni mwa mamlaka za udhibiti wa ubora, wazalishaji katika viwanda vidogo na vikubwa, wajasiriamali, taasisi za elimu ya juu na utafiti, walaji na wadau mbalimbali wa viwango na ubora wa Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Washindi hao walitangazwa na kukabidhiwa zawadi mwishoni mwa wiki Makao Mkuu ya TBS, jijini Dar es Salaam, ambapo mshindi wa kwanza alikuwa ni Maina Masole kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), ambaye alijinyakulia Sh. milioni 1,300, 000.

Shindano hilo la uandishi wa insha linalenga kuwajengea uelewa wanafunzi kuhusiana na masuala ya viwango ili waweze kuwa mabalozi wazuri ndani ya jamii.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa TBS, David Ndimalema, alisema zawadi zilitolewa kwa wanachuo walioshiriki katika uandishi wa insha iliyojikita katika kaulimbiu ya mwaka ya Siku ya Viwango Afrika isemayo;

"Nafasi ya uandaaji wa viwango katika kutangaza na kukuza sanaa, utamaduni na urithi-uchumi wa kiubunifu Afrika." Aliwapongeza waandaaji wa shindano hilo, kwani ushirikishwaji wa wanachuo ni njia mojawapo ya kueneza uelewa kuhusiana na matumizi ya viwango katika bidhaa na huduma mbalimbali.

Alisema kaulimbiu hiyo inawaelekeza katika tafakuri ya mchango wa viwango katika uchumi wa ubunifu kwenye sekta ya sanaa, utamaduni na urithi.

Alifafanua kuwa insha za washindi zitapelekwa kushindanishwa na insha za washindi katika nchi nyingine za Afrika na hivyo kusaidia kutangaza nchi yetu katika ngazi ya Bara.

# Shule zasaidiwa madawati, mabati

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE za msingi sita za mkoa wa Tanga zimewezeshwa kwa kupatiwa madawati 250 na mabati 170 vyenye thamani ya Sh. milioni 30.

Lengo ni kuwasaidia wanafunzi kukaa katika madawati, kutokana na awali wakisoma huku wamekaa chini.

Shule zilizopata msaada huo uliotolewa na Benki ya NMB ni Msambiazi ambayo ndiyo pekee imepata mabati. Nyingine ni Kwakombo zote zikiwa Halmashauri ya Mji Korogwe, na Mwisho wa Shamba iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe. Pia Mkata, Manga na Zavuza zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Akizungumza kwenye hafla mbili tofauti za makabidhiano zilizofanyika Shule ya Msingi Kwakombo wilayani Korogwe na Shule ya Msingi Mkata, Wilaya ya Handeni, Meneja wa NMB Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro, alisema misaada wanayotoa kwenye jamii, ni sehemu ya faida ya asilimia moja kwa mwaka inayopata kutoka kwa jamii hiyo.

Muro alisema benki hiyo imewekeza kwenye jamii kwa kufanya shughuli mbalimbali katika jamii, na hasa sekta za elimu na afya, na wameweza kwenda kwenye sekta hizo sababu ni mtambuka na zina changamoto nyingi, na kila wanapotoa msaada huo, kwao ni sehemu ya mchango wao kwa Taifa sababu inasaidia kusogeza maendeleo ya wananchi mbele, kwani ili nchi iweze kuendelea kunahitajika elimu na afya iliyo njema.

"Serikali, tunafahamu jitihada mnazofanya ni kubwa katika kuboresha Sekta ya Elimu. Lakini sekta hiyo ina changamoto nyingi. Na elimu ndiyo msingi wa maisha. NMB ikiwa kama mdau, inatambua jitihada za serikali, na sisi tumeweza kuona tuungane na serikali katika kutoa mchango wetu kwa jamii. Kila mwaka NMB inatenga asilimia moja ya faida, na huu ni mwaka wa nane (8) inafanya hivyo kila mwaka. Na NMB imejikita kwenye elimu na afya kutokana na umuhimu wa sekta hizo. Lakini pia, hata kwenye majanga NMB inashiriki.

Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Kissa Kasongwa, alisema mwamko wa watoto ni mkubwa kwenye kusoma na kupata elimu. Na serikali ikipata wadau kama NMB inasaidia, sababu changamoto ni nyingi kwenye elimu.

# OSHA yawapa elimu kiwanda cha nondo

**Frank Monyo**

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) imetoa mafunzo maalum ya usalama na afya kwa wafanyakazi zaidi ya 90 wa kiwanda cha kutengeneza nondo cha PNP Industries Limited kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujilinda dhidi ya ajali na magonjwa yanayotokana na mazingira yao ya kazi.

Akizungumza mkoani Dar es Saalam, baada ya mafunzo hayo yaliofanyika katika kiwanda hicho kilichopo Mikocheni, Mwezeshaji wa Mafunzo hayo kutoka OSHA, Respicious Kundawa, alisema mafunzo hayo ni muhimu hususan kwa wafanyakazi wanaohusika moja kwa moja katika mchakato mzima wa uzalishaji wa bidhaa hiyo muhimu.

"Katika mafunzo ya leo tumewalenga wafanyakazi katika viwanda vya kuzalisha nondo ambao tunafahamu wanakabiliwa na vihatarishi mbalimbali katika mlolongo mzima wa uzalishaji wa bidhaa husika kuanzia wanapopokea vyuma chakavu, kuvichambua, kuviyeyusha, kutengeneza nondo zenyewe na hata kuzipakia katika magari tayari kwa kuzisafirisha kwenda kutumika," alisema Kundawa na kuongeza kuwa;

"Katika hatua zote hizo mfanyakazi anaweza kutumia hivyo ni muhimu kuwapa wafanyakazi nyenzo za kujilinda."

Kwa upande wa uongozi wa kiwanda hicho umeeleza kuridhishwa na mafunzo yaliyotolewa na OSHA na kuahidi kuyafanyia kazi maelekezo yaliyotolewa kupitia mafunzo hayo.

"Tunashukuru OSHA kwa mafunzo waliyotupatia kwa siku ya leo ambayo yatatusaidia sana katika kuboresha mazingira yetu ya kazi pamoja na namna ambavyo tunafanya kazi," alisema Iddy Hamis, Ofisa Rasilimali Watu wa kiwanda hicho.

## Uzalishaji mgodi wa Mwadui kuendelea

WIZARA ya Madini imesema itafanya kila linalowezekana kuhakikisha mgodi wa Mwadui unaomilikiwa na Kampuni ya Williamson Diamond Limited (WDL), unaendelea na shughuli zake kama kawaida.

Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Kishapu (CCM), Boniphace Butondo.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji juu ya mgodi huo kushindwa kufanya kazi na kupelekea watumishi kupata tatizo la mishahara.

Alisema wapo watumishi zaidi ya 1,200 kwenye mgodi huo na tatizo kubwa la hao watumishi ni mishahara yao kusimama kwa muda mrefu.

"Sasa ipo sababu ya serikali kuona umuhimu wa mgodi huu ili kuhakikisha unaanza uzalishaji na hatimaye adha na matatizo makubwa ya watumishi waondokane nayo," alieleza mbunge huyo.

Akijibu swali hilo, Prof. Manya alisema wanapozungumzia uzalishaji wa almasi nchini moja kwa moja wanazungumzia WDL hivyo ni lazima jitihada zifanyike za kurudisha uzalishaji katika mgodi huo.

"WDL ndio kiini cha almasi hapa nchini na tunatambua adha ambayo watumishi wanapata kwa kushindwa kulipa mishahara, lakini tunatambua kuwa kama uzalishaji hautafanyika muda mrefu maana yake hata shimo lile litaporomoka na hivyo kupelekea gharama ya kuja kuanzisha mgodi mara nyingine itakuwa kubwa sana," alisema.

Alimhakikishia mbunge kuwa wizara hiyo itafanya kila linalowezekana ili mgodi huo urudishe hali ya uzalishaji hata kwa kufanya ushawishi kwa benki au kukaa na watoa huduma ili wakubali kufanya hata kwa kukopwa na baadaye wazalishe na kuuza.

"Hata kuongea na Petra ili ikiwezekana basi turejee katika uzalishaji na mara tutakapoanza uzalishaji ina maana matatizo yote ya mbunge aliyoyainisha ya adha ya watumishi kutokulipwa pamoja na tozo ya huduma vyote vitakuwa vimepatiwa suluhisho," alisisitiza.

Awali, katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji ni kwa nini mgodi huo umesimamisha shughuli za uzalishaji wa almasi kwa muda mrefu sasa na ni lini mgodi huo utaanza uzalishaji tena.

Prof. Manya akijibu swali hilo alisema mgodi huo ulisimamisha shughuli za uzalishaji Aprili 2020 kutokana na kushindwa kumudu gharama za uzalishaji kufuatia anguko la bei ya madini ya almasi katika masoko ya dunia.

"Anguko la bei ya almasi katika soko la dunia lilisababishwa na athari za mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (COVID-19) mwishoni mwa mwaka 2019.

"Athari ya kuanguka kwa bei ya almasi kulisababisha bei ya wastani ya almasi katika mauzo ya mgodi huo kwa Machi 2020 kuanguka hadi kufikia Dola za Marekani 131.13 kwa karati, bei ambayo haikidhi gharama za uzalishaji wa mgodi huo," alisema.

Alifafanua kuwa, kwa mujibu wa makadirio ya mgodi huo wastani wa bei unapaswa kuwa angalau Dola za Marekani 208.00 kwa karati ili mgodi uweze kukidhi gharama za uzalishaji.

# Uzalishaji mbegu bora kutengewa bil. 10.6/-

BUNGE limeelezwa kuwa katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa mafuta nchini, katika mwaka 2021/22, serikali itawekeza Sh. bilioni 10.6 kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za mazao yakiwamo ya mbegu za mafuta.

Pia serikali itaimarisha miundombinu ya umwagiliaji na kupanua mashamba ya mbegu kwa Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), na mbegu hizo zitasambazwa kwa wakulima wa mikoa yote inayozalisha mazao hayo ukiwamo Mkoa wa Mara kupitia kwa ASA na wasambazaji binafsi.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Bunda (CCM), Mwita Getere.

Katika swali lake, Mbunge aliyehoji kinachosababisha uhaba wa mafuta nchini.

"Nini kinasababisha Tanzania kutokujitosheleza kwa mafuta ya kula na serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha mikoa yenye ardhi ya kutosha ya kuzalisha zao la alizeti hususani Mkoa wa Mara inatambuliwa rasmi na kupewa?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Bashe alisema mahitaji ya mafuta ya kula nchini yanakadiriwa kuwa tani 570,000 kwa mwaka.

Hata hivyo, alisema uzalishaji wa mafuta ya kula unakadiriwa kufikia wastani wa tani 205,000 na kufanya upungufu wa wastani wa tani 365,000 kwa mwaka.

Alibainisha kuwa upungufu huo husababisha nchi kutumia wastani wa Sh. bilioni 474 kuagiza mafuta ya kula kutoka nje kwa mwaka.

"Uhaba wa mafuta ya kula nchini umetokana uzalishaji mdogo wa mazao ya mbegu za mafuta yakiwamo alizeti, michikichi na pamba unaochangiwa na matumizi hafifu ya teknolojia ikiwamo mbegu bora na usindikaji," alisema.

Alibainisha serikali inaendelea kuhamasisha kilimo cha mazao ya mafuta ikiwamo alizeti, michikichi na pamba katika mikoa yote yenye ardhi na hali ya hewa inayofaa kwa kilimo cha mazao hayo.

"Serikali imeweka msukumo wa kuimarisha huduma za ugani nchini ambapo katika bajeti ya 2021/22, wizara imepanga kuwezesha maofisa ugani 680 wa mikoa ya Singida, Dodoma na Simiyu pikipiki kwa ajili ya ufuatiliaji," alisema.

Kadhalika, alisema kupatiwa mafunzo rejea na kuwezesha wagani hao kuanzisha mashamba ya mfano ya alizeti na pamba pamoja na kuanzisha mashamba ya pamoja.

"Lengo la uwezeshaji huu ni kuleta ufanisi katika kutoa huduma za ugani ili kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya mafuta," alisema.

Alisisitiza kuwa serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuingia kwenye uzalishaji wa mbegu na ipo tayari kufanya majadiliano na kampuni au watu wenye nia ya kuwekeza kwenye uzalishaji wa mbegu ili kuweka utaratibu wa kupunguza gharama na kuzalisha mbegu kwa tija.



Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, akijadiliana jambo na Mbunge wa Jimbo la Mlalo, Rashid Shangazi, ndani ya ukumbi wa jijini Dodoma jana kwenye vikao vya bunge la bajeti vinavyoendelea. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Tozo 273 zilizokuwa kero kwa wawekezaji zafutwa

SERIKALI imesema tozo 273 ambazo zilikuwa kero kwa wawekezaji zimefutwa.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, William Ole Nasha, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Lupembe(CCM), Edwin Swalle.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuvutia wawekezaji katika kilimo cha parachichi mkoani Njombe.

Akijibu swali, Ole Nasha alisema serikali ya awamu ya sita imedhamiria kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini na ufanyaji wa biashara kwa kushughulikia kero zitokanazo na ukadiriaji na ukasanyaji wa kodi usio rafiki.

"Nyingine ni upatikanaji mgumu wa ardhi unaochukua muda mrefu kwa ajili ya uwekezaji, changamoto za upatikanaji wa vibali vya kazi na ukaazi na kuondoa tozo mbalimbali ambazo ni kero katika Serikali za Mitaa," alisema.

Alisema katika kutekeleza Sera ya Uwekezaji, serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kutoa vivutio kama vile misamaha ya kodi kwenye makasha-majokofu yanayotumika kuhifadhia mazao ya bustani ikiwemo zao la parachichi.

Aidha, alisema serikali ina mpango wa kujenga chumba baridi katika uwanja wa ndege wa Songwe, ambapo ndege za kimataifa zinazobeba mizigo zitaanza kusafirisha parachichi na mazao mengine ya matunda na mbogamboga moja kwa moja kwenda kwenye masoko ya kimataifa.

Vilevile, alisema serikali imepanga kujenga jengo lijulikanalo kama ukanda wa kijani katika Bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya kuhifadhi bidhaa/mazao yanayoharibika mapema ikiwamo zao la parachichi.

Alitaja jitihada nyingine ni kutafuta masoko ya nje, kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora, kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji, uhifadhi, uchukuzi na usafirishaji.

Alisisitiza kuwa serikali itaendelea kushirikiana na wadau wote ikiwamo sekta binafsi katika kukuza uwekezaji wa zao la parachichi.

Awali, alisema hadi kufikia mwaka 2020, thamani ya zao la parachichi katika soko la dunia inakadiriwa kuwa Dola za Kimarekani milioni 4,800.

"Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara, soko la parachichi linakadiriwa kuwa na thamani ya dola za Kimarekani milioni 254, nchi yetu imeendelea kufanya vizuri katika uzalishaji na uuzaji wa zao la parachichi katika masoko ya ndani na ya kimataifa kama vile Umoja wa Ulaya, China, India na Kenya.

"Mwaka 2020 kiasi cha Dola za Marekani milioni 8 kilipatikana kutokana na wastani wa kiasi cha tani 4,000 zilizosafirishwa katika soko la kimataifa," alisema.




Habari zote na Augusta Njoji

Nipashe
# TESA
Jumanne Mei 11, 2021
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

Mbinu udhibiti uharibifu wa vifaa umeme hizi



Ukurasa 12

Wenye ulemavu kumekucha mkopo Manispaa wawapaisha



Ukurasa 13

**Vigingi hivi vinawakwamisha wanaojifungua kurudi shuleni**

SAYANSI

**NA MWANDISHI WETU**

# Ndivyo Tanzania ilivyobahatika kuviepuka vimbunga na tufani



Athari za kimbunga katika baadhi ya miji duniani. **PICHA: MTANDAO**

LICHA ya kimbunga cha kitropiki cha jobo kuelezwa kuwa kingepiga pwani ya Tanzania na kusababisha maafa ukanda wa pwani, taarifa za watabiri wa hali ya hewa kimataifa zinasema ni nadra kutokea tufani hizo kwa vile Tanzania si mkondo wa vimbunga.

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), mwezi uliopita taifa lingeandika historia, ni ya kimbunga jobo ambacho kingeipiga Zanzibar, Mafia, Dar es Salaam na mikoa ya Lindi na Mtwara.

Kuhusu kimbunga hicho kutofika nchini, ilielezwa kuwa ni Tanzania si ukanda wa tufani za baharini kwa kuwa iko karibu na Ikweta ambao ni mstari wa 'kufikirika' unaoitenganisha dunia katika vipande viwili, kizio cha Kaskazini na cha Kusini.

Kitaalamu inaelezwa kuwa, kuwa jirani na Ikweta huleta faida kadhaa kama mvua nyingi na misimu miwili ya masika na mvua, jua la kutosha na pia kutofikiwa na vimbunga.

Kwa mujibu wa mtandao wa televisheni ya CNN ya Marekani, ni nadra kutokea vimbunga Tanzania na kwamba si taifa la dhoruba wala kimbunga kutokana na ukaribu wake ni mstari wa Ikweta ambako nguvu za uvutano za ' Coriolis force' zinazosababisha kuanzisha upepo mkali na dhoruba ili kuchochea vimbunga kuzunguka na kupata kasi kubwa ni dhaifa au hazina nguvu eneo hilo.

CNN inasema taarifa zilizopo kuhusu historia ya vimbunga vilivyoikumba Tanzania zinaeleza kuwa vilitokea mara mbili tangu karne ya 19 vikionyesha kuwa kulikuwa na kimbunga cha Zanzibar cha mwaka 1872-"Zanzibar Cyclone" of 1872 na cha Lindi mwaka 1952 kikiitwa Cyclone Lindi of 1952.

"Vimbunga hivyo viliikumba Tanzania miaka 80 kuanzia 1872 hadi 1952. Vikitokea Aprili 14, 1872 na kingine kikizuka Aprili 15, mwaka 1952."

Kwa mujibu wa CNN kuanzia wakati huo hadi leo takribani miaka 70 iliyopita hakuna maafa ya vimbunga tena.

Hata hivyo, kutokana na uelekeo wa kimbunga kutokea baada ya miaka 80 huenda jobo ulikuwa mwendelezo wa tufani zinazoikumba pwani ya Tanzania kila baada ya miaka 80.

Kutokana na utabiri huo, Lindi na Zanzibar yanabakia kuwa maeneo au mikondo ya vimbunga ambavyo hutokea mwezi Aprili ambao ni kilele cha mvua za masika nchini. Kuanzia mwaka 2019, vimbunga vya kitropikia 'idai na Kenneth' viliipiga Msumbiji na kusababisha maafa makubwa na maelfu ya watu kupoteza maisha huku uwekezaji ukiharibiwa kwa kiasi kikubwa tena kupindukia.

Kimbunga jobo ambacho kitaalamu huitwa 'tropical cyclone' kinaelezwa kuwa kinapatikana karibu na visiwa vya Madagascar kusini mwa Bahari ya Hindi.

Kimbunga ambacho ni upepo mkali mno wenye kasi na nguvu kubwa mara nyingi ukianzia baharini kuelekea pwani na kuelekea nchi kavu, kinaambatana na mvua kubwa. Wakati mwingine kasi ya upepo inapokuwa kubwa kupindukia na kimbunga hicho huitwa dhoruba.

Jobo ni kimbunga cha kitropiki kinachozalisha upepo mkali na mvua nyingi na kinahusishwa na tropiki au joto kwa sababu huanzia kwenye joto la takribani nyuzi 22 na kwa mwaka huu kikielezwa kuwa kilianzia kwenye nyuzi joto 29 na kwamba hali za kimazingira zingekizuia kisiendelee kuwa na nguvu na athari kubwa zaidi kwa kufika nchi kavu hasa mikoa ya ukanda wa pwani.

Hofu ya kukumbwa na kimbunga hicho kilichotangazwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilikuwa kubwa zaidi kwa wakazi wa mikoa ya ukanda wa pwani ya kusini inayohusika mikoa ya Lindi na Mtwara. Aidha, kilitarajiwa kufika Zanzibar, Bagamoyo pamoja na Dar es Salaam.

Hata hivyo, hofu ilitoweka baada ya kimbunga jobo kiichotarajiwa kilichokuwa kiwasili nchini Jumapili Aprili 25, kutangazwa na TMA kuwa kilitoweka na hakipo tena kutokana na kupungua nguvu na kufifia wakati kilipowasili katika ukanda mkavu wa pwani ya Tanzania.

**ATHARI ZA VIMBUNGA**

Msumbiji ni jirani na Tanzania na imekuwa na majanga mengi ya vimbunga yakiwamo matukio 46 ya vimbunga na mafuriko katika kipindi cha miaka 30 iliyopita. Majimbo yaliyoathirika ni pamoja na Cabo Delgado, Nampula, Manica, Zambezi na Sofala.

Kwa mujibu wa Taarifa za Umoja wa Mataifa (UN), idadi ya watu waliokufa kutokana na kimbunga idai nchini Msumbiji, Zimbabwe na Malawi ilifikia zaidi ya 615.

Taarifa zilizotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la uratibu wa misaada ya kiutu (OCHA) mwaka 2019 zilisema watu 417 walikufa nchini Msumbiji,139 Zimbabwe na 59 Malawi hata hivyo serikali ya Msumbiji ilisema pengine watu 1,000 walihofiwa kufa.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Wenye ulemavu kumekucha mkopo wa Manispaa wawapaisha



Mmoja wa wanachama wa kiwanda cha kutengeneza viatu akiwa kazini. **PICHA: MARCO MADUHU**

SERA ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2004, inauelezea ulemavu kuwa ni changamoto aliyonayo mtu kwenye viungo au kiakili. Anaweza kuzaliwa nayo, kuipata kwa kuugua au kutokana na ajali, kwa hiyo mtu yeyote ni mlemavu mtarajiwa.

Hata hivyo, ulemavu si kushindwa maisha kwa vile tiba yake ni kupata vifaa visaidizi na kuwezeshwa iwe kimtaji, teknolojia, elimu au kimiundombinu hatua inayowawezesha wanaoishi na ulemavu kujikwamua na kumudu maisha yao.

Ndivyo wanavyothibitisha wana kikundi cha Mapambano na Ufundi cha wanaoishi na ulemavu cha Manispaa ya Shinyanga, wanaojihusisha na kutengeneza viatu.

Hawa ni miongoni wa wanufaika na mikopo ya halmashauri ambao wanapata asilimia mbili, wakati kinamama na vijana wanapata asilimia nne kila kundi.

Wana Mapambano mwaka jana walinufaika na mkopo wa Shilingi milioni 10.2 na kufungua kiwanda kidogo cha kutengeneza viatu vya ngozi.

> Ilielekeza kuwa asilimia 10 za vijana na wanawake zigawanywe pia kwa wenye ulemavu kwa kupewa asilimia mbili.

Mweka hazina wa kikundi hicho John Samweli, akizungumza na Nipashe kwa niaba ya mwenyekiti wake, anasema awali kabla ya kupata mkopo huo, maisha yao yalikuwa magumu na walikuwa wakiishi kwa kushona viatu vilivyochanika na kupata pesa kidogo isiyokidhi mahitaji yao.

Anasema baada ya kusikia kuna pesa za mikopo asilimia mbili kwenye halmashauri kwa ajili ya watu wenye ulemavu, ndipo wakajiunga kwenye kikundi cha watu watano na kuanzisha mradi wa kutengeneza viatu.

Walinufaika na mkopo huo wa halmashauri na wamefungua kiwanda hicho cha viatu vya ngozi.

Anasema: "Tunaishukuru serikali kwa kututambua wenye ulemavu na kuanza kutupatia mikopo sababu tutakuwa tumesahaulika na kuonekana ni watu wa kupewa misaada wakati tuna uwezo mkubwa wa kufanya kazi na kujipatia mapato. Kikubwa kinachopaswa ni kuwekewa miundombinu rafiki na kuwezeshwa."

"Ukiangalia sisi maisha yetu yamebadilika na siyo tegemezi wala watu wa kuomba msaada, bali tuna uwezo wa kiuchumi na tunahudumia familia zetu, hivyo tunaiomba serikali iendelee kuwajali zaidi wanaoishi na ulemavu na kuwapatia mikopo ili tujikwamue kiuchumi," anaongeza Samweli.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu mkoani Shinyanga (SHIVYAWATA) Richard Mpongo, anasema fedha za mikopo za halmashauri zimekuwa msaada mkubwa kwa wanachama wake na kuwainua kiuchumi.

Anasema baadhi ya watu wenye ulemavu wana uwezo mkubwa wa kufanya kazi, lakini kilichokuwa kikiwakwamisha ni ukosefu wa mitaji pamoja na elimu ya ujasiriamali, na baada ya kuanza kupatiwa vitu hivyo wengi wanajishughulisha na biashara mbalimbali na kujipatia kipato.

"Tunaishukuru serikali kwa mpango wake wa kutoa fedha za mikopo kwa wenye ulemavu, ambazo zimetukomboa kiuchumi, mfano Halmashauri ya Ushetu imetoa fedha kwa vikundi vitatu, Msalala vitatu, Kahama Manispaa 12, Shinyanga Manispaa Sita, Kishapu na Shinyanga Vijiji kikundi kimoja kimoja," anasema Mpongo.

Anawaomba maofisa maendeleo wa halmashauri waendelee kutoa elimu hiyo ya mikopo na ujasiriamali kwa watu wenye ulemavu, kwa sababu wengi hawana uelewa ili kuwasaidia kujua namna ya kujikwamua kiuchumi na kuendesha maisha yao bila ya kutegemea misaada, anaongeza Mpongo.

Joseph Masota, mkazi wa Manispaa ya Shinyanga, anasema watu wenye ulemavu baadhi yao wana uwezo mkubwa wa kufanya kazi, lakini kutokana mitazamo potofu iliyojengeka ndani ya jamii kuwa wao ni tegemezi na hawana uwezo wa kufanyakazi, wamekoseshwa fursa na kuishi maisha magumu.

Anaitaka jamii kuelimika na kubadilika kuwa watu wenye ulemavu ni kama binadamu wengine, hivyo wapewe fursa mbalimbali ambazo zitawafaya kujiongizia kipato na kuacha kuwa tegemezi au kuomba misaada, sababu wengine wana uwezo mkubwa.

"Tumeshuhudia baadhi ya watu wenye ulemavu ambao wamewezeshwa, namna wanavyofanya kazi ya kujiingizia kipato, na hili jambo lingeanza toka zamani la utoaji mikopo, wange kuwa mbali sana na wala tusingeweza kuona omba omba mitaani," anaongeza Masota.

Ofisa Vijana Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga Charles Ruchagula, anasema fedha za mikopo za halmashauri asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu, walianza rasmi kuzitoa mwaka 2019 baada ya serikali kutoa mwongozo.

Ilielekeza kuwa asilimia 10 za vijana na wanawake zigawanywe pia kwa wenye ulemavu kwa kupewa asilimia mbili.

Anasema tangu mwaka huo 2019 mpaka mwaka jana, wameshatoa fedha za mikopo kwa watu wenye ulemavu kwa vikundi sita na kutoa jumla ya Sh. milioni 21.1 na wamekuwa wakiwatembelea ili kuona maendeleo yao, na wanafanya vizuri na kubainisha kuwa mwaka huu watatoa tena fedha hizo za mikopo.

Anawataka wenye ulemavu, kujitokeza kwa wingi kujiunga kwenye vikundi vya ujasiriamali, pamoja na kubuni mawazo bora ya kibiashara ambayo yatavutia mikopo na kuwasaidia kujikwamua kiuchumi na kuacha kuishi maisha magumu.

ELIMU

NA RAHM SULEIMAN, ZANZIBAR

# Vigingi hivi vinawakwamisha wanaojifungua kurudi shuleni

MIMBA za utotoni na hasa za wanafunzi shuleni ni tatizo la kitaifa, lakini kwa upande mwingine linawaumiza zaidi familia za watoto maskini.

Ndiyo mwanzo wa mtoto mkubwa kumlea mwenzake mdogo wakati hayo yanatokea mama mlezi huyo aliyetakiwa kuwa shuleni, bado hajajua njia bora za malezi kwa vile hata mwenyewe hajahitimu mafunzo ya kulelewa na wazazi wake.

Lakini, mbali na hayo mimba za utotoni zinaathiri afya na maendeleo ya kielimu ya mtoto na hatimaye kuvuruga maisha yake na hata ya huyo mtoto au watoto aliowazaa akiwa na umri mdogo.

Taarifa mbalimbali duniani zinaonyesha kuwa wasichana wengi hulazimika kwa sababu mbalimbali kukatisha masomo yao baada ya kupata ujauzito.

Hali inakuwa mbaya zaidi kwa watoto ambao ni raia wa nchi zenye sheria kali zinazowazuia wanafunzi kuendelea na masomo wakishagundulika kuwa wana mimba.

Sababu nyingine ya kukimbia masomo ni kuona aibu, kudhalilishwa, kuzomewa, kunyanyaswa na kufanyiwa kila aina ya karaha ambazo humkosesha raha hata kumkwamisha kuendelea na masomo.

### VIPI ZANZIBAR?

Hali ya kusikitisha pia ipo Zanzibar na kila mwaka Wazanzibari wanashuhudia wanafunzi wengi wa kike wakikatisha masomo kutokana na kupata ujauzito.

Licha ya sheria ya elimu ya Zanzibar kuruhusu wanafunzi wa kike wanaopata ujauzito kuendelea na masomo, lakini bado kiwango cha wanafunzi wanaorudi darasani ni wachache kutokana na sababu mbalimbali.

Kubwa zaidi linalowafanya wanafunzi hawa kutorudi shuleni kuendelea na masomo baada ya kujifungua ni unyanyapaa katika jamii na zaidi kwa wanafunzi wenzao.

Takwimu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali zinaonyesha wanafunzi 646 walipata ujauzito kutoka mwaka 2005 hadi 2020 Unguja na Pemba nakati yao 190 walikuwa kati ya miaka 13 na 16. Katika kipindi hicho cha miaka 15, wanafunzi 179 walikuwa wa shule za Unguja na 77 Pemba.



Waziri wa Elimu, Prof. Joyce Ndalichako. **PICHA: MTANDAO**

### CHANGAMOTO WANAZOKUTANAZO

Asha Ali (sio jina lake) mwenye miaka 15 aliyepata ujauzito akiwa kidato cha pili anaeleza alivyoshindwa kurudi shuleni kutokana na kutohimili unyanyapaa uliopo katika jamii.

Anasema anayepata ujauzito huonekana na jamii amefanya kosa kubwa bila kujali aliipata hali hiyo katika mazingira gani, kwani hata mwanafunzi aliyebakwa na kupata mimba anapewa hukumu hiyo inayomuumiza kama licha ya kwamba alinyanyaswa.

Anaongeza kuwa hiyo sio haki kwa sababu ni sawa na kutonesha kidonda kibichi.

"Ni kweli sheria inaniruhusu kurudi shule niendelee kusoma, lakini nashindwa, naona aibu na kuumizwa nilipoona jamii inaninyooshea kidole cha kunilaani kwa vile nimepata ujauzito utotoni," anasema kwa masikitiko.

Jambo jingine linalomkwaza hata kama angeamua kurejea shuleni ni kushindwa kusoma kutokana na msongo wa mawazo uliotokana na ujauzito.

Vile vile hali ya kiuchumi katika familia yake ni ndogo na kwa hivyo inamlazimu kuhangaika nje ya shule kupata riziki ili kumlea mwanawe.

Anayosema Asha, yamewakumba wanafunzi wengi wa Zanzibar wanaopata ujauzito na hata kusababisha baadhi yao huchukua uamuzi magumu ikiwamo kujiua kutokana na kushindwa kuvumilia matukano.

Msichana mmoja ambaye ni miongoni mwa wanafunzi wachache waliorejea masomoni baada ya kujifungua na kumaliza kidato cha sita anaeleza kwamba haikuwa kazi rahisi kuendelea na masomo.

Mwanafunzi huyo alipata ujauzito akiwa kidato cha pili na kuendelea na masomo mpaka karibu na kujifungua na akarudi darasani kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

"Nilipata ujauzito nilipobakwa na jirani yangu ambaye amekimbia na hadi sasa hajulikani alipo, lakini nawashukuru wazazi wangu kwa kunifariji, wakanishajiisha niendelee na masomo na kubeba jukumu la kumlea mwanangu," anasema binti huyo.

Anaongeza kuwa siyo wazazi wote wanaofanya kama wake hata wakiwa na uhakika kwamba mtoto wao alibakwa au alifanyiwa hadaa au kusababisha ulaghai uliopelekea mimba.

> Takwimu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali zinaonyesha wanafunzi 646 walipata ujauzito kutoka mwaka 2005 hadi 2020 Unguja na Pemba nakati yao 190 walikuwa kati ya miaka 13 na 16.

Anasema aliporudi shuleni alikabiliwa na unyanyapaa, lakini aliikabili kwa utulivu na ujasiri na hatimaye waliofanya hivyo wakajirekebisha taratibu kwa vile waliona hakutetereka na kujali zaidi masomo.

Anaongeza kuwa alipowasilisha ripoti ya tathmini ya utekelezaji wa sera ya wanafunzi kuendelea na masomo baada ya kujifungua katika mkutano wa wadau wa elimu, Mshauri Abdullah Khamis, anasema takwimu zinaonyesha wanafunzi wengine wanaopata ujauzito huogopa kurudi shule kutokana na kunyanyapaliwa na jamii na shuleni pia.

"Wazee wakiwafariji watoto wao kwa kuwapa ushauri mzuri katika kipindi cha ujauzito inawasaidia sana waliofikwa na mtihani huu kurudi shule kuvitumia vipaji vyao na hatimaye kutimiza malengo yao."

"Kupata ujauzito isiwe ni sababu ya kukatisha ndoto za baadaye za mwanafunzi, lakini ni muhimu kwa jamii kuachana na unyanyapaa na ihamasishe wanafunzi waliopata ujauzito kurudi shule ili kuwa na wigo mpana wa kupata watalaamu," anaongeza.

Jambo jingine linalofaa kupewa umuhimu ni kujua chanzo cha watoto kupata ujauzito wakiwa masomoni ili kuandaa mikakati ya kulimaliza tatizo hilo.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, anawataka wakurugenzi na wakuu wa vitengo vya wizara hiyo kutoa elimu kwa jamii kuhusu kuwarejesha shule wanafunzi waliopa ujauzito baada ya kujifungua.

Waziri anaitaka jamii kuacha tabia ya kuwanyanyapaa wasichana wanaopata ujauzito wakiwa masomoni kwani nao wanayo malengo ya kuwa wataalamu wazalendo katika taifa lao.

Mkurugenzi Tirso Dossantos, anayeliongoza Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni (UNESCO) anaahidi kuendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuwasaidi watoto kupata haki yao ya elimu.

Ofisa Mradi Sekta ya Elimu na Afya wa UNESCO Zanzibar, Hasina Salum Bukheit, anasema Wizara ya Elimu Zanzibar katika sera yake imetoa fursa ya kurudi masomoni kwa wanafunzi wanaopata matatizo mbalimbali, ukiwamo ujauzito.

TEKNOLOJIA

NA SABATO KASIKA

# Mbinu udhibiti uharibifu wa vifaa umeme hizi hapa



Rais wa Energy Control System, Jeff Edwards (kushoto) na Ofisa Masoko wa East African Sine Tamer, Samson Odera, wakizungumzia kifaa cha kudhibiti uharibifu unaoletwa na umeme. **PICHA: SABATO KASIKA**

TEKNOLOJIA ambayo ni maarifa na ujuzi wa kisayansi unaotumika katika kutatua na kuboresha maisha ya watu, iwe kwa njia ya mashine,vifaa na mitambo inazidi kupanuka na kugundua mambo mapya yanayoongeza ustawi katika jamii.

Zama hizi ubunifu unazidi kupanuka katika nyanja nyingi ukiwamo ujio wa vifaa mbalimbali kwa mfano vya umeme, vinavyotumika kulinda mifumo ya umeme ili kupunguza uharibifu wa vitu viwe vya nyumbani au viwandani pale hitilafu inapotokea, lengo likiwa ni kuviacha salama na kupunguza dosari zisizo zinazoepukika.

Kifaa kinachokabiliana na nguvu ya umeme inapoongezeka kwa kuizuia isiunguze vifaa kama jokofu, runinga, redio nyumbani na jenereta, viyoyozi na mifumo ya kompyuta viwandani ni mojawapo ya manufaa ya ugunduzi huo.

Kifaa hicho kinatajwa pia kuwa ni mahiri kumaliza tatizo kwenye mfumo wa usafirishaji wa umeme hadi unapowafikia watumiaji, ni kwa mujibu wa Ofisa Masoko wa kampuni ya Sine Tamer East Africa, Samson Odera.

Anasema ugunduzi huo unalenga kuzihimiza taasisi za umma na binafsi na wateja binafsi kufunga kifaa hicho cha Sine Tamer Black Box ili kulinda mifumo ya umeme na kupunguza uharibifu na hasara inapotokea hitilafu.

> “Hii ni teknolojia mpya iliyovumbuliwa na wataalamu kwa manufaa hata kwa shule zenye nishati hiyo, ili kuepusha tatizo la ukatikaji ovyo wa umeme.

Katika mazungumzo na gazeti hili wakati wa kutambulisha kifaa hicho jijini Dar es Salaam hivi karibuni, anasema wanaunga mkono hatua za serikali za kuipatia Tanzania umeme wa kutosha kwa maendeleo.

“Kumekuwapo na tatizo la umeme kuongezeka ghafla ‘power upsurges’ na wakati mwingine kuwapo na umeme mchafu ‘transient’, kutokana na sababu mbalimbali na kusababisha athari...”

Anasema ili kulinda vifaa hivyo iwe viwandani au nyumbani ni muhimu kuweka mifumo hiyo ili kuwa salama, anaongeza Odera.

Ujio wa kifaa hicho unakuja wakati serikali imefanya jitihada mbalimbali kuongeza umeme ili kuwapatia wananchi nishati ya kutosha kuanzia majumbani, taasisi za umma na binafasi na hata viwandani.

Katika jitihada za kuboresha nishati nchini, inajenga bwawa la umeme la Nyerere au Stigler’s linalotarajiwa kuzalisha megawati 2,100 za umeme utakaotumika kuanzia majumbani, viwandani na hata kuuza ziada nje.

Lakini, pamoja na serikali kufanya jitihada hizo za kuboresha huduma na kuongeza upatikanaji wa umeme, lipo tatizo linalotatiza jitihada hizo, ambalo ni uwezo wa kulinda vifaa vinavyotumia nishati hiyo.

### KWA NINI?

Anasema kuna haja ya kuwa na Sine Tamer Black Box ili kuepusha uharibifu na kwamba jitihada hizo zimelenga kuwasaidia wateja wa makundi yote wanaotumia umeme.

“Kwa kushirikiana na kampuni ya Energy Solution tunatoa huduma ya kifaa hicho kulinda mifumo ya umeme kuanzia majumbani, taasisi mbalimbali za huduma, viwandani na popote tunapohitajika,” anasema.

Ili kuepusha uharibifu huo kampuni yao inaendelea kutilia mkazo ndoto za serikali ya awamu ya tano ya kutaka kuwa na Tanzania ya viwanda ifikapo mwaka 2025, kwa kuhimiza ufungaji wa kifaa hicho ili kuepusha madhara.

“Hii ni teknolojia mpya iliyovumbuliwa na wataalamu kwa manufaa hata kwa shule zenye nishati hiyo, ili kuepusha tatizo la ukatikaji ovyo wa umeme,” anasema.

### UFUNGAJI

Ofisa masoko huyo anasema, hadi sasa tayari wameshafunga vifaa hivyo kwenye baadhi ya viwanda, taasisi za fedha na katika maeneo mengine nchini ili kukabiliana na uharibifu unaoweza kusababishwa na hitilafu ya umeme kuongezeka ghafla.

“Tumefunga katika Ofisi za Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali, Hospitali ya Taifa Muhimbili na katika benki kadhaa ikiwamo NMB na CRDB na tunaendelea kufanya kazi hiyo kwa wale ambao wanahitaji huduma yetu,” anasema.

Anafafanua kuwa Tanzania kama mataifa mengine yaliyopitia hatua hiyo ya msingi ya mapinduzi katika teknolojia, kampuni yao imeona kuna haja ya kusaidia kuimarisha huduma ya nishati kwa kuleta kifaa hicho.

Anasema, wao wameamua kuja na teknolojia hiyo, ambayo wanaamini kuwa iwapo taasisi, nyumba na viwanda zitafunga kifaa hicho, hitilafu za umeme zitapungua na hivyo kuwa na manufaa katika shughuli za maendeleo.

“Tunataka kuhakikisha tunatoa mchango, sio tu kuwa na mtazamo wa kuona mafanikio makubwa kwa kutumia teknolojia hii mpya, bali pia kuelekeza njia za kuondoa vikwazo vinavyosababisha umeme kuwa na hitilafu,” anasema.

### VIPI GHARAMA?

Mwanzilishi na Rais wa Kampuni ya Energy Control System (ECS), Jeff Edwards, kutoka Texas Marekani, anasema, kifaa hicho na kinasaidia upunguzaji wa gharama za matumizi ya ukarabati wa mitambo.

“Baadhi ya vifaa kama balbu, zinaungua kutokana na umeme kuja kwa kasi au kuwa na uchafu, hivyo kampuni yangu iko tayari kushirikiana na East African Sine Tamer kuhakikisha tatizo hilo linaisha nchini,” anasema Edwards.

Hivi karibuni, Rais huyo alikuwa jijini Dar es Salaam akishirikiana na East African Sine Tamer kuelezea umuhimu wa kifaa hicho, kwa lengo la kuhimiza matumizi ya kifaa hicho ili kuboresha huduma mbalimbali.

“Kufunga kifaa hicho kunapunguza gharama za matengenezo ya umeme kwa asilimia 80 na kupata faida zaidi, hivyo ni muhimu nchi kuwa na umeme ambao mifumo yake inalinda na kutunza vifaa mbalimbali vinavyotumiwa kwenye uzalishaji,” anasema.





# Sababu wawekezaji kuitwa kuwekeza Dodoma zatajwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetoa wito kwa wawekezaji kuwekeza jijini Dodoma kutokana na ujio wa serikali kuongeza mahitaji ya huduma za kijamii.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kuzindua rasmi Hoteli ya nyota nne ya Rafiki Dodoma Hoteli.

Alisema wawekezaji wanahitaji katika Jiji hilo kutokana na uwepo wa shughuli nyingi za kiserikali na kitaifa ambazo zinahitaji uwekezaji katika huduma mbalimbali.

Alisema hoteli hiyo itasaidia kupunguza tatizo la nyumba za kulala wageni zenye hadhi ambazo zinahitajika hivi sasa kwa wingi jijini humo.

"Kupatikana kwa hoteli hii katika Jiji la Dodoma itatusaidia kuondoa usumbufu uliokuwapo hapo awali hasa wakati wa mikutano mikubwa ambayo wageni walikuwa wanapata shida kupata sehemu ya kulala zenye hadhi," alisema Prof. Mkenda. Aidha, alisema kuwa wawekezaji wote ambao wanataka kuja kuwekeza katika Jiji la Dodoma milango ipo wazi kwa kuwa serikali itasaidia kufanikisha uwekezaji wao ili kusaidia kutoa ajira kwa makundi mbalimbali. Alisema hivi sasa serikali imeweka mazingira wezeshi kwa mtu yeyote ambaye atahitaji kuja kuweza katika sekta mbalimbali.

Naye Mbunge wa Dodoma, Anthony Mavunde, alisema kuwa jiji hilo limejipanga kuhudumia wawekezaji ambao wataonyesha nia ya kuwekeza katika sekta mbalimbali.

Mavunde alisema kuwa hivi sasa kupitia Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya jiji hilo wameweka mikakati ya kuhudumia wawekeza kwa muda mfupi na kuwapatia maeneo ya uwekezaji bila urasimu.

"Moja ya faida ya uwekezaji kama huu hapa jijini Dodoma ni kubadili mwonekano wa jiji letu, lakini uwepo wa hoteli kubwa kama hivi kunasaidia kuondoa uhaba wa nyumba za kulala wageni hasa wakati ule tunapokuwa na mikutano mikubwa," alisema.

Mkurugenzi wa hoteli hiyo, Fladimiry Mallya, alisema kuwa wameamua kuja kuweza katika jijini humo kutokana na fursa zilizopo hivi sasa.

Hata hivyo, aliiomba serikali kuwashika mkono wawekeza katika kuwasaidia kukabiliana na kero mbalimbali ambazo wamekuwa wakikumbana nazo.



Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Profesa Devis Mwamfupe (katikati), akiwasikiliza wajasiriamali katika siku ya uzinduzi wa kijiji kipya uliofanyika Dodoma jana. PICHA: PETER MKWAVILA

# Kituo cha kupozea umeme kukamilika kabla ya Desemba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Nishati, imesema itahakikisha mradi wa upanuzi wa kituo cha kupozea umeme kilichopo Bwawa la Mtera, unakamilika kabla ya Desemba mwaka huu, ili kusaidia kusambaza umeme katika vijiji ambavyo bado havijapata huduma hiyo.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alitoa kauli hiyo juzi katika ziara ya kikazi kwenye kituo hicho cha kuzalisha umeme cha Mtera.

Byabato alisema gharama za ujenzi wa mradi huo ni Sh. bilioni saba huku akisema ujenzi wake ulisimama kutokana na sababu mbalimbali zilizo nje ya uwezo wao.

"Nimekagua upanuzi wa mradi huo unaendelea vizuri, nimekagua pia mgodi na sehemu ya kutoa umeme, katika mitambo ambayo ina mapanga yanayozunguka kwa ajili ya kuzalisha umeme," alisema Byabato.

Alisema katika upanuzi wa kituo hicho wamepanga kuongeza megawati 20 zaidi ili kuhakikisha kituo hicho kinatoa umeme wa kutosha ili maeneo ya Mpwapwa na Iringa Vijijini nao wapate umeme huo.

Kuhusu kina cha maji kwenye bwawa hilo, Naibu Waziri huyo alisema kimejaa na hata mvua isiponyesha maji yaliopo yana uwezo wa kuzalisha umeme ndani ya mwaka nzima.

"Hata mvua zisiponyesha tunaweza kuzalisha umeme kwa mwaka mzima kwa hiyo jamii isiwe na wasiwasi katika suala zima la upatikanaji wa huduma ya nishati kutoka katika kituo hichi cha Mtera," alisema.

Alisema serikali inaendelea na uboreshaji wa miundombinu ya kupeleka umeme kwa wananchi ambapo kabla ya Desemba mwaka huu awamu ya pili ya mzunguko wa tatu wa umeme wa REA inayoendelea na ujenzi itakuwa imekamilika. "Lakini muda wa mkataba kwa mkandarasi umeongezwa ambapo ameagiza kuhakikisha REA wanasimamia hilo ili mradi huo ukamilike kabla ya Desemba jamii iweze kutumia...hakikisheni watu wanafanya kazi usiku na mchana, tunahitaji kuona mradi huo unakamilika kwa haraka," alisema.

Kwa upande wake, Meneja wa kituo hicho, Mhandisi Eliasi Mwalupilo, alisema serikali itaanza kufanyia matengenezo mtambo huo ili ukamilike kama ilivyopangwa.

Alisema hivi sasa maji yapo ya kutosha bwawani na wananchi watarajie huduma nzuri ya umeme kutoka katika kituo hicho cha Mtera.

Naye Mhandisi John Nzorotu, Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi REA, alisema mradi huo ulisimama ujenzi kutokana na kusubiri vifaa ambavyo vimeshafika.

# NMB yadhamini mashindano ya sayansi, ubunifu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MASHINDANO ya kitaifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu yamepata udhamini.

Udhamini huo umetolewa na Benki ya NMB ambayo imetoa shilingi milioni 15 kwa ajili ya udhamini ya mashindano hayo yaliyofunguliwa rasmi jijini Dodoma.

Fedha hizo zilikabidhiwa na Mhazini Mkuu wa benki hiyo, Azizi Chacha, ambaye alisema fedha hizo ni udhamini wa mashindano hayo yanayondaliwa na Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Chacha alibainisha kuwa lengo la NMB kusaidia fedha hizo ni kuisaidia serikali katika kufanikisha mashindano hayo ya kitaifa ambayo yamekuwa na malengo ya kuibua wabunifu wapya kila mwaka .

Alisema benki hiyo inashiriki katika mashindano hayo kwa kuwa ni wadhamini na wamekuwa wakiwasaidia baadhi ya wabunifu katika kufanikisha ndoto zao za kuendeleza ubunifu huo kwa kuwapa mikopo .

Alibainisha kuwa kuna baadhi ya wabunifu wamekuwa na miradi ambayo inaajiri watu wengine, hivyo wakiwezeshwa watatoa ajira zaidi kwa vijana na makundi mengine.

Kadhalika, alisema NMB imekuwa ikishirikiana na serikali katika mashindano hayo kila mwaka ili kuhakikisha wabunifu wapya wanaibuliwa kila mwaka kwa lengo la kulisaidia taifa.

Aidha, alisema NMB inamilikiwa na serikali kwa asilimia 38, hivyo ni jukumu la benki kuiunga mkono serikali katika kuwezesha miradi na mipango mizuri iliyokusudiwa.

Kwa upande wake, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, aliwashukuru Benki ya NMB na wadau wengine kwa kuwaunga mkono katika mashindano hayo kwa kutoa kiasi hicho cha fedha.

Prof. Ndalichako aliwaomba benki hiyo kuendelea kudhamini mashindano hayo ambayo yamekuwa yakifanyika kila mwaka kwa washiriki kufanya maonyesho kwa wiki moja.

Aliongeza kuwa serikali itaendelea kutenga bajeti zaidi ili kuhakikisha mashindano hayo yanafanyika kwa lengo la kuibua wabunifu wapya kila kona ya nchi.

Alisema mashindano hayo yanashirikisha wabunifu kutoka vyuo vya ufundi, shule za msingi, vyuo vikuu na wabunifu binafsi kutoka maeneo mbalimbali.



# TFS yapiga jeki ujenzi wa daraja

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Shamba la Miti Kiwira, limetoa msaada wa saruji mifuko 100 na nondo rola 78, wenye thamani zaidi ya milioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa daraja lilipo Kijiji cha Ngumburu Kata ya Isongole wilayani Rungwe.

Akikabidhi msaada huo juzi, Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti Kiwira, Lucas Sabida, kwa Mkuu wa Wilaya ya Rungwe na wananchi wa Kijiji hicho, alisema waliamua kusaidia baada ya kuona wananchi wanaozunguka shamba hili kupata adha ya usafiri wanapokwenda shambani au kusafirisha mazao.

Alisema kutokana na uhusiano mzuri walionao na wananchi wanaozunguka shamba hilo, waliamua kuchangia shughuli za ujenzi wa daraja hilo ili kuwaondolea adha ya usafirishaji wa mazao, wanafunzi na wajawazito ambao kipindi cha masika hushindwa kupita kwenye daraja hilo ambalo lilijengwa kwa miti.

"Shamba la miti Kiwira tumekuwa na mahusiano mazuri na majirani zetu ambao wanazunguka shamba hili tunasaidiana katika nyakati zote kwa kutambua umuhimu huo tunaendelea kuwasaidia kuboresha na kujenga miundombinu mbalimbali ya kutolea huduma za kijamii vikiwamo vituo vya kutolea huduma, shule pamoja na ujenzi wa daraja ambao tumechangia," alisema Sabida.

Alisema TFS inatambua mchango mkubwa unaotolewa na wananchi hasa vijiji vinavyozunguka mashamba ya miti ya kupandwa na kwamba katika kuliona hilo kupitia mpango wake kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imeweka mikakati mbalimbali ya kuchangia shughuli za maendeleo.

Aliongeza kuwa ushirikiano huo unalenga kuimarisha mapambano dhidi ya majanga ya moto yanayoweza kujitokeza hasa kipindi cha kiangazi.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, aliishukuru TFS Kiwira kwa msaada huo na kwamba wamekuwa mstari wa mbele kuwasaidia wananchi kwenye shughuli za maendeleo.

Chalya alisema mifuko 100 ya saruji pamoja na nondo walizotoa zitasaidia kukamilisha haraka ujenzi wa daraja la kudumu katika Kijiji cha Ngumburu.

Alisema serikali itaendelea kuomba misaada mbalimbali kwa TFS kutokana na mahusiano mazuri waliyonayo.

Aidha, Chalya aliuagiza Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kusimamia na kutoa ushauri wa kitaalamu kwenye ujenzi wa daraja hilo.

Alisema TARURA wawajibike kusimamia ili daraja likamilike kwa wakati huku ujenzi ukizingatia ubora na viwango vinavyohitajika badala ya kuwaachia wananchi pekee kuendelea na ujenzi.

Wananchi wa Kijiji cha Ngumburu, walisema kuwa ubovu wa daraja hilo ulikwamisha kusafirisha mazao yao ambayo wanayatoa shambani kupeleka sokoni.

Miongoni mwa wananchi hao, Justine Moses alisema kwa muda mrefu sasa wamekuwa wakipata adha ya usafiri kutumia daraja hilo ambapo wanafunzi hushindwa kupita wanapoenda shuleni, wakulima kushindwa kusafirisha mazao pamoja na wajawazito.

Alisema msaada huo utakuwa utasaidia kumaliza haraka ujenzi wa daraja la kudumu ambalo litaondoa vikwazo vilivyokuwa vinawakabili.

Diwani wa Isongole, Mwalingo George, alisema kutokana na adha walizokuwa wakizipata wananchi juu ya daraja la Ngumuru waliamua kuchanga nguvu kazi zao ambazo ni ufyatuaji wa matofali na fedha.

# Wawekezaji Mbarali wakumbushwa sheria

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, amewataka wawekezaji wilayani humo kufuata sheria na miongozo ya uwekezaji.

Miongoni mwa mambo hayo ni kushiriki shughuli mbalimbali za kijamii ambazo ni ujenzi wa shule, vituo vya kutolea huduma za afya na uboreshaji wa miundombinu ya maji.

Mfune alitoa kauli hiyo jana wakati wa ziara ya kamati ya ulinzi na usalama iliyofanyika kwenye kata za Chimala na Ilongo na kusema wawekezaji wapya wa maghala na wenye viwanda vya kuchakata zao la mpunga wanapaswa kufuata na kuzingatia kanuni za uwekezaji sambamba na kujenga uhusiano mzuri na wananchi wanaozunguka maeneo hayo.

Alisema wamiliki wa viwanda vya kuchakata zao la mpunga msimu huu wa mavuno wanapaswa kupanua wigo wa ajira wa vijana sambamba na kuendelea kuboresha miundombinu ya uwekezaji ili kuifanya wilaya hiyo kuwa kitovu cha zao hilo.

Alisema wawekezaji wakiboresha miundombinu ya maghala wakulima watavutiwa na kwenda kuhifadhi mazao yao kwani watakuwa na amani mazao yao kuwa salama.

"Tuko kwenye msimu wa mavuno, tunahitaji kuwa na maghala ya kisasa ili wakulima waweze kuhifahi mazao yao katika hali ya usalama nawaomba mwendelee kuboresha ili kukuza mazingira ya uwekezaji," alisema Mfune.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wawekezaji hao walisema wamekuwa wakipata ushirikiano mzuri na uongozi wa Wilaya pindi wanapohitaji ushauri na vibali vya kujenga maghala maeneo mengine.

Walisema kupitia viwanda vya kusindika mpunga wamezalisha ajira kwa wananchi sambamba na kuwasaidia wakulima kuhifadhi mazao yao.

Aidha, waliishauri serikali kuendelea kuboresha sheria mbalimbali za uwekezaji na kupunguza baadhi ya tozo ambazo wakati mwingine zinawaumiza wawekezaji.



Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti Kiwira lililoko mkoani Mbeya, Lucas Sabida (kulia), akikabidhi mifuko ya saruji kwa Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Challya (wapili kushoto), kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Ngumburu. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Walimu wajengewa uwezo kukabili ujangili

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WALIMU wa masomo ya Jiografia na Maarifa ya Jamii wa Shule za Msingi na Sekondari wanaozunguka hifadhi za Kitulo na Katavi wamejengewa uwezo wa umuhimu wa uhifadhi na namna ya kutunza mazingira ili kukabiliana na ujangili.

Shirika la Hifadhi la Taifa (TANAPA) lilitoa mafunzo kwa walimu wa masomo hayo kutoka mikoa ya Njombe, Mbeya na Katavi ambao wanafundisha shule zilizoko pembezoni mwa hifadhi hizo ili kukabiliana na vitendo vya ujangili, ambapo kupitia elimu waliyoipata watawafundisha watoto umuhimu wa uhifadhi.

Hayo yalisemwa juzi na Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi nchini, Godwell Ole Meing'ataki, wakati wa kuhitimisha mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wa masomo ya Jiografia na Maarifa ya Jamii wanaofundisha shule zilizoko pembezoni mwa hifadhi.

Alisema walianzisha programu hiyo ili kuwafikia wanafunzi ambao hawatambui umuhimu wa hifadhi hizo hivyo kupitia walimu wao wataweza kuzilinda na kuzihifadhi.

Alisema jumla ya shule za msingi 23 na sekondari 13 kutoka Mikoa ya Njombe, Mbeya na Katavi zimenufaika na elimu ya kujengewa uwezo juu ya masuala mbalimbali ya uhifadhi.

Alisema programu hiyo ambayo kwa sasa ni kama rasimu italeta mwitiko chanya kwani itawafikia walengwa moja kwa moja hususani wanafunzi ambao watakuwa mabalozi wazuri wa wazazi wao na jamii kwa ujumla.

"Tuliamua kuanzisha programu hii kwa wadau wa elimu baada ya kubaini kuwa licha ya kuwa na ujirani mwema na shule zinazozunguka hifadhi, lakini bado hawana elimu ya kutosha juu ya umuhimu wa hifadhi zetu, kupitia mafunzo na shughuli mbalimbali tutakazozifanya kupitia programu hii itasaidia kukabiliana na vitendo vya ujangili pamoja na uharibifu wa mazingira kuzunguka hifadhi," alisema Ole Meing'ataki.

Alisema TANAPA inaendelea kutoa elimu kwa walimu kutoka maeneo mbalimbali nchini ambao wanafundisha shule zilizoko karibu na hifadhi ili jamii iendelee kutunza wanyama na uoto unaopatikana katika hifadhi sambamba na kukuza uhusiano mzuri wa ujirani mwema.

Zawadi Makinda, mhifadhi kutoka kitengo cha mawasiliano ya jamii, aliwataka walimu kuhakikisha maarifa waliyoyapata, wanawapa wanafunzi ili nao wakawe mabalozi wazuri kwenye familia na jamii zao kuhusu umuhimu wa uhifadhi.

Baadhi ya walimu walisema jamii nyingi hazijui faida za uwapo wa hifadhi katika maeneo yao kutokana na kuwapo kwa usimamizi mkali, hivyo kupitia mafunzo hayo watawaelimisha juu ya umuhimu wa ujirani mwema na kutunza hifadhi hizo kwa manufaa ya sasa na baadaye.








Mtoto Hasanati Khamis, akipokea zawadi ya ushindi katika Mashindano ya Kuhifadhi Quran, yaliyofanyika Viwanja vya Mao Zanzibar, yakiwa ya saba tangu yalipoasisiwa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni, Mhandisi Hamad Yussuf Masauni (wanne kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Corona yasababisha kituo kurekebisha tabia kuchelewa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUCHELEWA kuanza kutumika kwa kituo cha kurekebisha tabia kwa vijana wanaotumia dawa za kulevya kilichopo Kidimni, kumesababishwa na ugonjwa wa corona.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais, Dk. Sada Mkuya, wakati akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio, mapato na matumizi ya bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2021-2022. Alisema, kituo hicho kilitumika kwa ajili ya kuhifadhi wagonjwa wa maradhi ya corona na serikali kushindwa kuingiza fedha za ujenzi kwa wakati.

Alisema kituo hicho sasa kinatarajiwa kuanza kazi mwezi wa Julai, mwaka huu na kutumia Sh. bilioni 2.7 katika ujenzi wake.

Dk. Mkuya alisema kituo hicho cha kisasa cha kwanza katika ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kati kimejengwa kwa ajili ya kuwapatia matibabu vijana walioathirika na dawa za kulevya ili kuwarudisha katika hali yao ya kawaida.

Alisema matarajio ya serikali ni kupokea vijana kutoka Unguja na Pemba wapatao 50 kwa hatua ya awali kwa ajili ya kupata matibabu ya kuondokana na athari za matumizi ya dawa za kulevya.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wananchi kwamba kituo cha kurekebisha tabia kwa vijana kutibu athari za dawa za kulevya kiliopo Kidimni Wilaya ya Kati Unguja, ujenzi wake umekamilika na kinatarajiwa kupokea vijana mwezi Julai mwaka huu," alisema. Alisema zaidi ya Sh. bilioni 2.9 zinahitajika kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo hilo kwa awamu ya pili hadi ya tatu.

"Mheshimiwa Spika jengo la kurekebisha tabia kwa vijana walioathirika na matumizi ya dawa za kulevya limekamilika ghorofa ya kwanza na tayari kuhamiwa na tumeomba fedha kwa ajili ya ghorofa ya pili na tatu," alisema.

Pia alisema zaidi ya miaka mitatu Serikali ya Zanzibar imekuwa ikitoa huduma mbalimbali kwa nyumba zinazotoa huduma ya matibabu kwa vijana kuachana na dawa za kulevya. Alisema zaidi ya nyumba sita za watu binafsi zimepatiwa jumla ya Sh. 1,500,000 kila mmoja kwa ajili ya kusaidia kutoa huduma kwa vijana wanaopatiwa hifadhi ya tiba katika nyumba hizo.

"Kabla ya kuwapo kwa kituo kipya cha tiba kwa waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya huko Kidimni tayari serikali tumekuwa tukitoa fedha kwa ajili ya kuzisaidia nyumba binafsi za watu waliojitolea kwa ajili ya kuwapatia tiba vijana wetu," alisema.

# Miradi sita ya uwekezaji katika hatua za mwisho

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMLA ya miradi sita ya uwekezaji ikiwamo ujenzi wa viwanda na hoteli za kitalii katika eneo huru la uchumi la Micheweni-Pemba ipo katika hatua za mwisho za matayarisho ya kuanza kazi baada ya kuidhinishwa na Mamlaka Huru ya Uwekezaji (ZIPA).

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni-Pemba, Shamata Shaame Khamis, aliyetaka kujua ni miradi mingapi inayotarajiwa kutekelezwa huko.

Soraga aliitaja miradi inayotarajiwa kutekelezwa katika kisiwa cha Pemba ni pamoja na ujenzi wa kiwanda cha sukari pamoja na cha biskuti.

Alikitaja kiwanda kingine kinachotarajiwa kujengwa katika eneo hilo kuwa ni pamoja na cha kusarifu na kuongeza thamani ya zao la mwani.

Alisema serikali imekitangaza kisiwa cha Pemba kuwa ukanda maalumu wa uwekezaji na mchakato wa kukamilisha kwa baadhi ya tozo ambazo lengo lake kuwavutia wawekezaji upo katika hatua za mwisho.

"Napenda kumjulisha mwakilishi wa Jimbo la Micheweni kwamba tayari serikali ipo katika mchakato wa kutayarisha mwongozo wa kanuni za tozo ambazo zitasaidia kuwavutia wawekezaji kuwekeza katika eneo la ukanda maalumu wa uwekezaji huko Micheweni Pemba," alisema.

Aliitaja mikakati mingine inayokusudiwa kuchukuliwa kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji ni kujenga miundombinu ya majisafi na salama, nishati ya umeme pamoja na barabara zinazokwenda katika maeneo ya wawekezaji.

# Vijana 58 wapata mafunzo utafiti nishati mafuta, gesi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Abdalla Hussein Kombo, amesema jumla ya vijana 58 wamepatiwa elimu ya masuala ya utafiti wa nishati ya mafuta na gesi kwa ajili ya kufanya kazi katika sekta hiyo na kupatiwa mikataba maalumu wafanyakazi hao kuhakikisha hawakimbii nchini na kutafuta ajira nyingine.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae, Shaaban Ali Othman, aliyetaka kujua vijana wangapi wamepatiwa masomo ya elimu kuhusu masuala ya mafuta na gesi pamoja na utafiti.

Waziri Kombo alisema licha ya vijana hao kupata elimu hiyo, serikali inawapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wake kuhusu masuala ya mafuta na gesi ambayo Zanzibar ipo katika mchakato wa utafutaji wa nishati hiyo.

Alisema wizara pamoja na wanafunzi waliopata elimu ya juu nje ya nchi wamefikia makubaliano na kutia saini kwamba wataitumikia Zanzibar kwa kipindi chote.

Alisema hatua hizo zimechukuliwa kwa lengo la kudhibiti vijana hao wasikimbie nchi na kutafuta ajira nyingine huku serikali ikiwa tayari imetumia fedha nyingi kusomesha vijana hao.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefikia makubaliano na vijana wote waliopatiwa ufadhili wa masomo nje ya nchi kuhakikisha elimu waliyoipata wanaitumia Zanzibar ambapo tumefanya hivyo ili kuepuka tabia ya baadhi ya wanafunzi hao kukimbia nje," alisema.

Alisema serikali imetayarisha muundo wa maslahi ikiwamo mishahara kwa watumishi wa kada ya mafuta na gesi ambayo ni mpya kwa sasa huku mahitaji yake yakiwa ni makubwa kufuatia Zanzibar kuanzisha mchakato wa utafiti wa mafuta na gesi.

Alisema yupo kijana mmoja ambaye amesomeshwa na serikali masuala ya mafuta na gesi nje ya nchi tayari anatafutwa na serikali baada ya kutoonekana kazini kwa zaidi ya miezi mitatu sasa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SUZAN JEREMIAH** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0248-0110** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **MARIAN GIRLS HIGH SCHOOL** mwaka 2013,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **WMB/RB/289/2021.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MESHACK RODGERS NSARO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0723/0088** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary BOLOTI mwaka 2019 ,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/KIG/RB/117996/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ROONEY KRISEN KONGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0444-0101** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ITAMBA mwaka 2009,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/URA/RB/231645/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO BOMANI (W) YA IRINGA**

**(MCA/84) R; 2002**

**SHAURI LA MADAI NO 18/2021**

**MDAI: ..............................ANASTASIUS MBOGORO**

**MDAIWA: ......................1. HUSSEN BACHU**
**2.MARIA RASTEL LYIMO**

**Shauri hili la madai tajwa hapo juu limefunguliwa katika mahakama hii na mdai mtajwa hapo juu akimtaja mdaiwa mtajwa hapo juu fedha shilingi 7,000,000/-**

Wadaiwa popote pale mlipo mnaamriwa na mahakama hii kuhudhuria Mahakamani

tarehe 20/05/2021 saa 2:30 bila kukosa siku hiyo,kwaajili ya kujibu madai hayo. Na kwa

kuwa siku hiyo ni siku ya kusikiliza shauri hilo, ni lazima kuleta nyaraka na ushahidi wote

kuhusiana na shauri hilo kwaajili ya kujitetea. Usipofika bila taarifa shauri litasikilizwa

upande mmoja na kutolewa hukumu

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 06/05/2021

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi NO.97/2021**

**Ombi la LUSIA COSMASI MKUDE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu COSMAS WILLIAM MKUDE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 04/05/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe12/04/2021

Tarehe 12/04/2021
Sahihi ya Hakimu
Mahakama ya Mwanzo Mjini
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**PAUL MOSES CHAPAULINGE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 450 BUR** AINA YA **BOXER**.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/237484/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THE REGISTERED TRUSTEES OF THE ROMAN CATHOLIC DIOC.-RURENGE** Wanatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T168AKS** aina ya MITSUBISH PAJERO Rangi yenye Chasis **No.CHNV340PJ00799** Engine **No.4D56FK7695.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **NGR/RB/5221/2021**


***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Kenya kuchunguza shutuma unyanyasaji kijinsia

**Nairobi,** KENYA

MAOFISA wa Polisi Kenya, wanachunguza kisa cha polisi wa kike kulalamika juu ya dhuluma na unyanyasaji wa kijinsia, kwenye video iliyosambaa mtandaoni.

Kwenye video hiyo, ofisa huyo anauliza aruhusiwe kujiuzulu kwa amani kutoka kwenye huduma hiyo, akisema alikuwa ameandika barua nyingi za kujiuzulu.

Ofisa huyo alisema barua hizo zilikuwa bado hazijafika kwa mkuu wa polisi, Inspekta Jenerali Hilary Mutyambai.

Ofisa huyo aliye katika mji wa pwani wa Mombasa alielezea kufadhaika kwake juu ya ukosefu wa haki na ufisadi na kitengo cha Mambo ya Ndani cha polisi, ambacho kinashughulikia malalamiko dhidi ya polisi.

Alisema hali hiyo ya kufadhaika muda mrefu huwa kati ya sababu za baadhi maofisa wa polisi kujiua au kuua wengine. **BBC**

## Walinda amani UNAMID waomba hifadhi Sudan

**Khartoum,** SUDAN

SHIRIKA la kuhudumia Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR), limethibitisha kwamba walinda amani wa zamani, wameomba hifadhi nchini Sudan.

Walinda amani wa zamani takribani 120 kutoka Ethiopia mahali ambapo mikoa kadhaa ikiwamo wa Kaskazini wa Tigray, imeathiriwa na mzozo wa kikabila, wanatafuta hifadhi nchini Sudan, UN, ilisema Jumapili.

Wafanyakazi walipangiwa kurudishwa nyumbani kama sehemu ya kuondoka kwa awamu kwa tume hiyo ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa (UNAMID), kutoka mkoa wa Darfur, Magharibi mwa Sudan baada ya mamlaka yake kumalizika Desemba 31.

"Kufikia sasa walinda amani 120 wa zamani wa UNAMID ambao walilazimika kurudishwa wameomba ulinzi wa kimataifa," msemaji wa walinda amani wa UN, aliliambia shirika la habari la AFP kupitia barua pepe. **VOA**

# Waasi 10 wauawa Mashariki mwa Congo

**Kinshasa,** DRC

WAASI 10 wameuawa na silaha zao sita kukamatwa na jeshi, wakati hali ya dharura ikitangazwa katika mikoa ya Kivu ya Kaskazini na Ituri.

Wakati huo huo, ujumbe wa jeshi la Uganda umewasili Beni katika maandalizi ya operesheni za pamoja kati ya jeshi la Uganda na Congo.

Rais Felix Tshisekedi, siku yake ya tano zilizopita alitangaza, wanajeshi wa DRC walikabiliana na waasi wa ADF katika mji mdogo wa Halungupa.

"Tumeona na kuhesabu maiti kumi ya wapiganaji wa ADF na kukamata silaha ya kawaida AK-47," alisema Meleki Mulala, msemaji wa jeshi la Congo.

**Rais Felix Tshisekedi, siku yake ya tano zilizopita alitangaza, wanajeshi wa DRC walikabiliana na waasi wa ADF katika mji mdogo wa Halungupa.**

Mafanikio hayo ya majeshi ya Congo dhidi ya waasi wa ADF, yalipokelewa kwa shangwe kubwa na mashirika ya kiraia ya sekta ya Ruwenzori kwa namna ya pekee na yale ya wilaya na mji wa Beni kwa ujumla.

Majeshi ya Congo yalisema yana uwezo wa kupambana na ADF.

Akizungumza na DW, Meleki Mulala, mwenyekiti wa mashirika ya kiraia maarufu Nouvelle société civile katika sekta ya Ruwenzori, aliwaomba wakazi kuliunga mkono kikamilifu jeshi la Congo, ili kuhakikisha amani ya kudumu inarudi Ruwenzori.

Waasi wa ADF wakiwa kabla na baada ya kutangazwa kwa hali ya dharura na Rais Tshisekedi waliendelea kuvishambulia vijiji, kuwaua watu pamoja na kupora mali, majeshi ya Congo nayo yalisema yana uwezo wa kupambana na ADF hadi pale watakapotokomezwa.

"Tumejipanga sawasawa ili tusonge mbele na kuwatokomeza hawa watu. Lengo letu nikurudisha amani kwa nguvu, ili amani hiyo tuwapatie raia wetu, ili raia wa Beni wajisikie huru kuishi katika eneo ambalo mnapatikana amani ya kudumu," alisema Anthony Mualushayi, msemaji wa FARDC jeshi la Congo katika eneo la Beni na Butembo.

Kwa kipindi cha miezi minne, majeshi ya serikali ya Congo yamedai kuwaua waasi wa ADF zaidi ya 100 na kuwakamata zaidi ya 50, kwa mujibu wa mashirika ya kutetea haki za binadamu, yanayofuatilia kwa karibu operesheni hizo dhidi ya ADF. **DW**



Wapalestina wakikimbia mabomu ya kutoa machozi wakati wakikabiliana na vikosi vya usalama vya Israeli katika kiwanja cha Msikiti wa Al Aqsa kwenye Jiji la Kale la Jerusalem jana. Wapalestina wasiopungua 180 walijeruhiwa katika ghasia hizo na 80 kulazwa hospitalini. **PICHA: AP**

# Maofisa watano wauawa kwa bomu Mogadishu

**Mogadishu,** SOMALIA

MLIPUKO ulisababishwa na mshambuliaji wa kujitoa mhanga na kujilipua jirani na maofisa nje ya kituo cha wilaya ya Waberi, amesababisha vifo vya maofisa watano.

Kwa mujibu wa mashuhuda tukio hilo lilitokea majira ya saa tatu usiku kwa saa za huko.

Maofisa hao ni miongoni mwa watu wasiopungua sita waliouawa Jumapili jioni.

Meja Sadiq Aden Ali, msemaji wa jeshi la polisi la Somalia, alithibitisha kwa vyombo vya habari kuwa makamanda wawili wa polisi ni miongoni mwa waliouawa.

Meja Ahmed Abdullahi Bashane, Kamanda wa Wilaya ya Waberi na Meja Abdibasid Mohamud Agey, naibu kamanda wa zamani wa idara ya polisi ya Weliyow Adde, waliuawa pamoja na maofisa polisi wengine watatu.

Raia mmoja ambaye alikuwa akiishi karibu na kituo hicho cha polisi pia aliuawa katika mlipuko huo.

Watu sita wengine walijeruhiwa katika mlipuko huo, kulingana na taarifa ya polisi.

Shahidi ambaye hakuweza kutajwa jina lake kwa sababu za kiusalama, alisema Bashane alikufa katika eneo la tukio wakati Agey alifariki kutokana na majeraha aliyopata baada ya kuondolewa kwenda sehemu nyingine kwa matibabu.

Saa tatu kabla ya mlipuko huo, Bashane alituma ujumbe wa 'Mother's Day' akimtakia heri mama yake kwenye ukurasa wake wa Facebook. **VOA**




# BAYERN YAJITOSA SAINI YA SANCHO

**MUNICH,** Ujerumani

MABINGWA wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich wanafikiria kujitosa kwenye usajili wa mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, kwa mujibu wa The Telegraph.

Wakati msimu huu wa 2020-21 ukielekea mwisho, majaliwa ya Sancho yametawala vyombo vya habari.

Akiwa anatupiwa upatu wa kuondoka Borussia Dortmund mwanzo mwa msimu huu, nyota huyo wa England ameendelea tena kutawala vichwa vya habari.

Na sasa Bayern Munich wanafikiria kujiunga kwenye mbio za kuwania saini ya mchezaji huyo wakati wa kipindi cha uhamisho wa majira ya joto.

Sancho kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na miamba wa Ligi Kuu ya England, Manchester United, pamoja na Liverpool na Chelsea.

# Pirlo akataa kujiuzulu Juventus

**TURIN,** Italia

ANDREA Pirlo hana mpango wa kujiuzulu pale Juventus baada ya matumaini ya 'Bianconeri' hao kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao kupatwa na pigo Jumapili.

Juve walikumbana na kichapo cha mabao 3-0 nyumbani kutoka kwa AC Milan na hivyo kupanda hadi nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Serie A, huku zikiwa zimebaki mechi tatu ligi kufikia mwisho, na kuwaweka kwenye wakati mgumu zaidi katika mbio za nne bora.

Imekuwa ni mara ya kwanza kwa Juve kukutana na kipigo cha nyumbani kutoka kwa 'Rossoneri' hao Machi 2011, huku pia wakiweka rekodi ya kuruhusu mabao mengi zaidi nyumbani dhidi ya Milan tangu Januari 2010.

Pirlo amekuwa na msimu mgumu tangu achukue mikoba ya kuinoa Juve kutoka kwa Maurizio Sarri.

Si tu ubabe wao wa kutwaa taji la ligi kwa misimu tisa mfululizo kuzimwa na Inter, lakini walitupwa nje hatua ya 16-bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Porto.

Wakati maamuzi juu yake bado hayajafikiwa, Pirlo amesisitiza hana mpango wa kujiuzulu kwenye nafasi yake hiyo.

"Hapana, sijajiuzulu," alisema akiiambia Sky Sport Italia. "Nilichukua nafasi hii nikiwa na malengo nao makubwa licha ya kupitia magumu."





# Zidane akasirishwa na penalti ya Sevilla

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane aliachwa na hasira kwa maamuzi ya Sevilla kupewa penalti baada ya Eder Militao kuunawa mpira eneo la hatari wakati Real Madrid ikilazimishwa sare ya mabao 2-2 na sasa inaonekana kama ubingwa haupo mikononi mwao.

Mchezo huo uliopigwa katika dimba la Alfredo Di Stefano juzi Jumapili, Madrid walikuwa nyuma kwa mabao 2-1 zikiwa simesalia dakika 10, kabla ya kusawazisha na kupata pointi moja.

Baada ya mchezo huo, Zidane alioonekna kukasirishwa na penalti hiyo na kusema kwamba haelewi kinachoendelea.

"Sielewi chochote. Kama Militao aliunawa mpira, Sevilla pia waliunawa mpira," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Sikufurahishwa na maamuzi ya mwamuzi (Juan Martinez Munuera). Kamwe huwa sizungumzii kuhusu waamuzi, lakini leo nina hasira.

"Mwisho wa siku ndivyo ilivyotokea, hatuwezi kubadili chochote. Nina furaha kuhusu mchezo wetu, tulistahili kushinda kwa sababu tulikuwa kwenye wakati bora zaidi.

"Siwezi kulizungumzia hilo tena. Tumeshazungumza kuhusu hilo. Waamuzi wanatakiwa kuelezea kwangu mimi, lakini ndio ilivyotokea. Tutakwenda kupambana hadi mwisho."

# KANE MIKONONI MWA CHELSEA




**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea imeingia kwenye mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, kwa mujibu wa jarida la Football Insider.

Chelsea wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 27, ambaye anahusishwa na Manchester United na Manchester City.

Kwa mujibu wa ripoti, Chelsea imepanga kumsajili Harry katika kipindi cha dirisha la uhamisho la kipindi cha majira ya joto.


Kane anaripotiwa kuwa na thamani ya zaidi ya pauni milioni 100, lakini imependekezwa atashinikiza kuondoka Spurs ili kutimiza azma yake ya kutwaa mataji.

Nahodha huyo wa timu ya Taifa ya England, mapema mwaka huu alibainisha wazi kuwa, atatoa hatima yake baada ya michuano ya euro 2020 inayofanyika Juni mwaka huu.

Mchezaji huyo ameweka wazi kwamba, anataka kupata changamoto mpya ambako ataweza kutwaa mataji.

Msimu huu Kane amecheza mechi 32 katika mshindano yote akiwa na Tottenham na kufanikiwa kufunga mabao 21 baada ya kuanza msimu akiwa majeruhi.

## Maguire hatihati fainali ya Europa



**MANCHESTER,** England

HARRY Maguire anaweza kukosa kuichezea Manchester United kwenye mchezo wa fainali ya Ligi ya Europa, baada ya kocha Ole Gunnar Solskjaer kusema nahodha huyo anaweza kuwa nje ya dimba kwa "wiki chache."

Maguire alipata maumivu kwenye mchezo wa Ligi Kuu England wakati Man United wakicheza na Aston Villa, juzi Jumapili.

Mlinzi huyo wa kati wa England aligongana na Anwar El Ghazi kwenye mchezo huo wa ushindi wa mabao 3-1 na nafasi yake ilichukuliwa na Eric Bailly dakika ya 78.

Na sasa kocha wa 'Mashetani Wekundu' hao, Solskjaer anasubiria kuona ukubwa wa jeraha la nyota huyo kabla ya mchezo wa fainali ya Europa dhidi ya Villarreal uliopangwa kupigwa Mei 26, mwaka huu.

"Matumaini yangu Harry anaweza kuwa fiti kwenye fainali," alisema Solskjaer. "Kwa sasa sijui sana. Tunatakiwa kuangalia upya. Inawezekana ikawa kwa wiki chache au miezi.

"Aliumia kwenye kigimbi cha mguu. Nafikiri mchezaji alimkanyaga au alimkwatua kwa nyuma."

## *Mourinho kuendelea kulipwa Spurs*

**LONDON,** England

JOSE Mourinho ambaye aliteuliwa na AS Roma kuwa kocha mpya wa klabu hiyo, wiki iliyopita, lakini ataendelea kulipwa na Tottenham Hotspur kiasi cha pauni milioni 10.

Mwalimu huyo alipata kazi mpya siku 15 tu baada ya kufutwa kazi na Tottenham.

Amesaini mkataba wa miaka mitatu na Waitaliano hao wenye thamani ya pauni milioni tano kwa mwaka - ikilinganishwa na pauni milioni 15 ya kila mwaka aliyokuwa akipata Spurs.

Lakini kama sehemu ya kukataliwa kwake, klabu hiyo ya London Kaskazini ilikubali kumlipa upungufu wa mshahara ikiwa angechukua wadhifa mwingine kwa mshahara wa chini kabla ya kumalizika kwa mkataba wake msimu ujao wa majira ya joto.

Hiyo inamaanisha wakati Mourinho atachukua madaraka kule kwenye dimba la Olimpico msimu huu wa majira ya joto, atapokea pauni milioni tano kutoka Roma na kwa msimu ujao tu, pauni milioni 10 kutoka Tottenham.

Lakini Spurs wameokoa pauni milioni tano kwa kile ambacho kingewagharimu kumlipa kwa siku zilizobaki katika mkataba wake.

Kocha huyo wa zamani wa Porto, Chelsea, Inter, Real Madrid na Manchester United, ana nia ya kuonyesha hana kosa wala kuathiriwa na kuondoka kwake kwa mshtuko baada ya miezi 17 tu ya uongozi.

Mourinho mwenye umri wa miaka 58, atachukua nafasi ya Mreno mwenzake, Paulo Fonseca.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GREENWOOD AIPIKU REKODI YA ROONEY

Ni ya kufunga mabao mengi zaidi Ligi Kuu England akiwa na umri wa miaka 19 ambapo...

**MANCHESTER,** England

MASON Greenwood ameweka rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi kwenye Ligi Kuu England akiwa na umri mdogo zaidi na kumpiku Wayne Rooney.

Greenwood alikuwa kwenye orodha ya wafungaji wa Man United wakati wakiifumua Aston Villa 3-1 juzi Jumapili na kuingiza kwenye rekodi mpya ya kufunga mabao mengi akiwa na umri wa miaka 19.

**Rooney alikuwa anashikilia rekodi ya kufunga mabao mengi (15) akiwa na umri wa miaka 19.**

Na sasa Greenwood amefikisha mabao 16 aliyofunga kwenye Ligi Kuu England akiwa na umri wa miaka 19. Greenwood iliifanya United iwe mbele kwa mabao 2-1 muda mfupi baada ya Bruno Fernandes kusawazisha kwa mkwaju wa penalti, wakati alipopokea pasi kutoka kwa Aaron Wan-Bissaka na kumzunguka Tyrone Mings kabla ya kupiga kwenye kona ya chini kulia.

Hilo lilikuwa bao la 16 kwenye maisha yake ya soka ya Ligi Kuu England, baada ya kupata la kwanza Novemba 2019 muda mfupi baada ya kutimiza umri wa miaka 18.

Greenwood anaweza kuongeza rekodi yake pia, kwani bado hajafikisha umri wa miaka 20 hadi itakapotimu Oktoba mwaka huu.

## ZISIKUPITE

### PSG YAKOMAA NA SALAH

KLABU ya PSG inajipanga kumsajili mshambuliaji wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah, 28, endapo straika wake, Kylian Mbappe ataamua kutokuongeza mkataba wake. ***(Mirror)***

### DRAXLER AONGEZA MKATABA

KIUNGO wa PSG na Ujerumani, Julian Draxler, 27, amekubali kuongeza mkataba wa mwaka mmoja na klabu hiyo kabla ya mkataba wake wa sasa kufikia tamati mwishoni mwa msimu. ***(Le Parisien)***

### MOURINHO AONYWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur wamemuonya kocha wao wa zamani, Jose Mourinho asijihangaishe kujaribu kuwasajili wachezaji wao wawili, Eric Dier, 27, na kiungo wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, 25, atakapoanza kuinoa klabu ya Roma msimu ujao.

### MSHIKO JUU KWA FERNANDES

KIUNGO wa Ureno, Bruno Fernandes anatarajiwa kupatiwa mkataba mpya ambao mshahara wake utapandishwa mara mbili kufikia pauni 200,000 kwa wiki na klabu yake ya Manchester United baada ya fainali ya Kombe la Ligi ya Europa. ***(Sun)***

### INTER KUMUUZA VIDAL

KLABU ya Inter Milan itapokea ofa za usajili kwa kiungo, Arturo Vidal, 33, kama sehemu ya mpango wa klabu hiyo kupunguza mlima wa mishahara. ***(Calcio Mercato)***

### AJAX WAMTAKA SULEMANA

AJAX inajiandaa kupambana na Manchester United kumpata winga wa Ghana, Kamaldeen Sulemana, ambaye sasa anaichezea FC Nordsjaelland ya Denmark. ***(Mail)***

### CAVANI KUBAKI UNITED

MANCHESTER United itampa mshambuliaji wa Uruguay, Edinson Cavani, 34, nyongeza ya mshahara wa pauni milioni 2.5 ili kumbakiza mchezaji huyo klabuni hapo kwa mwaka mwingine.***(Sun)***

### HODGSON KUMBAKISHA EZE

KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson, anaamini kuwa klabu hiyo itambakiza kiungo raia wa England, Eberechi Eze, 22, kwa msimu wa 2021-22 licha ya mchezaji huyo kuzivutia klabu mbalimbali. ***(Goal)***

### SANCHO AWEKEWA OFA

MANCHESTER United inaandaa ofa ya pauni milioni 80 ili kumsajili winga wa England anayechezea miamba ya Ujerumani klabu ya Borussia Dortmund, Jadon Sancho, 21. ***(Star)***

### WATFORD WAMTAKA BORRE

KLABU ya Watford ambayo ipo mbioni kupanda Ligi England, ipo katika mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji wa Colombia, Rafael Borre, 25, ambaye mkataba wake na miamba ya Argentina klabu ya River Plate unafikia tamati mwishoni mwa msimu. ***(Sun)***

## HABARI MICHEZO

# Iringa na sababu soka lao kushuka

**Na Zuhura Zukheir,** IRINGA

UKATA na kuyumba kiuchumi kwa baadhi ya wadau wa soka, kumetajwa kuwa sababu kubwa ya timu za Mkoa wa Iringa ikiwamo Lipuli FC, kutofanya vizuri hadi kushuka daraja hali ambayo imeuamsha Umoja wa Veterani mkoani hapa kutafuta mwarobaini wa kulinusuru soka la Iringa.

Akizungumza wakati wa bonanza la Iringa Combine Veterani, Katibu Mkuu wa Umoja wa Veterani Mkoa wa Iringa na Mratibu wa bonanza hilo, Pastor Kwambiana, alisema timu zote za mkoani hapa zimekuwa zikimtegemea mdhamini mmoja tu, Asas, ambaye naye amekuwa akielemewa kutokana na wingi wa klabu ambazo zote zinahitaji fedha.

Alisema uendeshaji wa timu za mpira wa miguu unahitaji fedha nyingi hivyo kumtegemea Asas peke yake kunaleta changamoto kubwa katika uendeshaji huku akitoa rai kwa wadau watakaoguswa kujitokeza kuzisaidia timu hizo.

"Sisi timu zetu zinakabiliwa na changamoto ya fedha ni ngumu sana kuendesha timu kwa kumtegemea mdhamini mmoja ambaye ni Asas, ndio ahudumie timu zote hapa ili tusimame tena ipo haja ya kila mmoja wetu kwa nafasi yake aone umuhimu wa kuzisaidia timu hizi," alisema Kwambiana.

Aidha, Kwambiana alisema jambo lingine linalochangia kuporomoka kwa soka ni kukosekana kwa umoja wa wadau wa soka na viongozi wa mpira pamoja na kuendekeza makundi na majungu hali inayosababisha klabu kukosa usimamizi mzuri.

**WEWEEE!...**



Msanii maarufu wa filamu nchini, Abdallah Makumbila (Muhogo Mchungu) akitaniana na msanii mwenzake, Nicole Berry (Kichuna), wakati wakitambulishwa kwenye hafla ya MultiChoice Tanzania iliyofanyika jijini Dodoma juzi, MultiChoice ilitambulisha mafanikio iliyoyapata na mchango wake kwa maendeleo na ustawi wa jamii ya Watanzania kwa mwaka uliopita. Hafla hiyo iliyoambatana na futari. **NA MPIGAPICHA WETU**

# NABI AIANDAA YANGA SC KUIANGAMIZA NAMUNGO

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuahirishwa kwa mechi yao ya watani wa jadi dhidi ya Simba, benchi la ufundi la Yanga, linaloongozwa na Kocha Mkuu Nasreddine Nabi, limesema sasa nguvu zao wanazielekeza katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, kocha huyo alisema wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya mechi yao ijayo, ugenini dhidi ya Namungo FC ambayo anahitaji kupata matokeo chanya.

**Alisema maandalizi yanaendelea vizuri na ana matumaini utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa kutokana na pande zote mbili kuhitaji kupata matokeo.**

"Maandalizi yanaendelea vizuri, tunajiandaa kwa ajili ya michezo yetu yote ikiwamo dhidi ya Namungo FC, tunafanyia kazi upungufu wetu hususan kujiimarisha kwenye safu ya ushambuliaji na viungo ili kwenda kutafuta matokeo chanya kwenye mchezo huo," alisema Nabi.

Naye kiungo wa Yanga, Haruna Niyonzima, alisema wamejiandaa vizuri kukabiliana na Namungo FC na utakuwa mchezo wa ushindani kwa sababu kila pande unahitaji matokeo mazuri.

"Suala la ubingwa kama nilivyosema awali kwamba, bado hatujaondoka katika mipango hiyo kwa sababu lolote linaweza kutokea kwa waliokuwa juu yetu kupoteza mechi na kukosa pointi na sisi tukafanya vizuri," alisema Niyonzima.

Yanga inayoshika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 57 zilizotokana na mechi 27, Jumamosi katika Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, itakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Namungo FC iliyopo nafasi ya 11 na alama zake 32 baada ya kushuka dimbani mara 24.





Meneja Mkuu wa Boomplay Tanzania, Natasha Stambuli (kulia), akikabidhi msaada wa vifaa tiba kwa Muuguzi Kiongozi Idara ya Nje ya Hospitali ya Mwananyamala, Henrietta Ishara. Msaada huo ulitolewa juzi jijini Dar es Salaam, Boomplay waliadhimisha Siku ya Mama Duniani kwa kutoa vifaa vya matibabu kwa Hospitali ya Mwananyamala, kuunga mkono juhudi za afya salama na ya uhakika kwa kina mama nchini. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Boomplay yageukia afya

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inarejesha kile inachokipata katika jamii, Kampuni ya Boomplay, App, inayoongoza barani Afrika kwa huduma ya kusikiliza na kupakua muziki imeadhimisha Siku ya Mama (Mother's Day) mwaka huu kwa kutoa vifaa vya matibabu kwa Hospitali ya Mwananyamala ili kuunga mkono juhudi za afya salama na ya uhakika kwa kina mama nchini.

Hospitali hiyo ya rufani jijini Dar es Salaam inahudumia wastani wa kinamama wajawazito 900 hadi 1,400 kwa mwezi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya makabidhiano iliyofanyika hospitalini hapo, Meneja Mkuu wa Boomplay Tanzania, Natasha Stambuli, alisema msaada huo ni sehemu ya utekelezaji wa mipango endelevu inayolenga kusaidia jamii.

"Tunayo furaha kutumikia jamii yetu na hasa katika siku hii ya kinamama duniani. Tunaelewa mchango na shida wanazopitia kinamama hasa wakati wa uzazi katika jamii zetu.

"Tunapowasherehekea kina mama, tunafurahi kuchangia msaada wetu na tunatarajia kufanya mengi zaidi kwenye jamii katika siku za usoni," alisema Stambuli.

Hamasa hiyo iliungwa mkono na Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Zavery Benela, ambaye aliisifu kampuni hiyo kwa msaada wake, na kuongeza kuwa umekuja katika muda muafaka wakati ambao ulimwengu unakabiliwa na changamoto ya huduma za afya.

"Kwa niaba ya hospitali nzima, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Boomplay kwa msaada huu wa huruma. Tuna hakika kuwa mchango wao utasaidia sana katika kuhakikisha huduma zetu za kinamama zinaendelea bila kukatizwa," alisema Dk. Benela.


Mpango huo ni mwanzo wa miradi mingine mingi ya jamii ambayo Boomplay inakusudia kuzindua katika siku za usoni.

"Kama kampuni, tunaendelea kujitolea kutekeleza jukumu letu katika jamii, kwa lengo la kuleta matokeo chanya na kuacha alama katika maisha ya wengi," alisema Stambuli.

# Michezo

Jumanne Mei 11, 2021

Nipashe

Greenwood aipiku rekodi ya Rooney UKURASA 22

MARATHON...



Mkurugenzi wa Mawasiliano Benki ya CRDB, Tully Esther Mwambapa (katikati), akiwa pamoja na klabu ya mbio za baiskeli ya Matambuu wakati wa hafla ya uzinduzi wa mbio za kimataifa za CRDB Bank Marathon 2021. Kulia ni Makamu wa Rais Chama cha Baiskeli Tanzania, Hussein Ally na Makamu Katibu wa Chama cha Riadha Tanzania, Ombeni Zavara (watatu kushoto). **NA MPIGAPICHA WETU**

# Gomes aeleza jeuri ushindi Kaizer Chiefs

## ●●● Waondoka leo alfajiri kuelekea Sauzi huku akitoa sababu ya kushinda nje ndani kuwa...

**Na Saada Akida**

KIKOSI kilichobeba dhamana ya kupeperusha bendera ya Tanzania, Afrika Mashariki na Kati kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kimekwekea pipa leo alfajiri kuelekea Afrika Kusini tayari kwa ajili ya mchezo wao wa robo fainali ya michuano hiyo utakaopigwa Jumamosi.

**Simba ambayo ni timu pekee kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati iliyosalia kwenye michuano hiyo, Jumamosi majira ya saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki itashuka katika Uwanja wa FNB jijini Johannesburg, Afrika Kusini, kuwavaa wenyeji wao, Kaizer Chiefs katika robo fainali ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa.**

Kwa mujibu wa uongozi wa klabu hiyo, mabingwa hao wa Tanzania walitarajia kuondoka leo alfajiri kuelekea Kenya wakiwa na kikosi cha wachezaji 27, huku msafara mzima ukitarajiwa kuwa na watu 40.

"Kikosi cha mabingwa wa nchi kitaondoka alfajiri ya Jumanne Mei 11, 2021 (saa 9:45) kuelekea Afrika Kusini kupitia Kenya tayari kwa mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Kaizer Chiefs utakaopigwa Jumamosi," ilieleza taarifa ya klabu hiyo.

Aidha, akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema anatarajia kuwapo kwa ushindani mkubwa katika mchezo huo, lakini anaamini wachezaji wake watafanya vizuri na kupata matokeo chanya.

Alisema analifahamu vema soka la Afrika Kusini na uzoefu huo anao, hivyo anaamini utamsaidia kuendelea kuandaa kikosi chake kwa ajili ya kwenda kutafuta matokeo chanya ili kuweza kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Nilipenda kukutana na Yanga kabla ya kucheza mchezo wa robo fainali dhidi ya Kaizer Chiefs, ili kuongeza utimamu wa wachezaji, lakini hilo limeshindikana na tunaendelea na maandalizi yetu kwenda kukabiliana na wapinzani wetu hao kufanya vizuri ugenini na kuja kutafuta ushindi nyumbani," alisema Gomes.

Alisema kutokana na uzoefu wa kulifahamu soka la nchi hiyo, ana matarajio makubwa kwa namna alivyokiandaa kikosi chake watahakikisha wanaenda kupambana kutafuta matokeo chanya katika mchezo huo wa ugenini.

"Malengo yetu ni kusonga mbele katika kila hatua, baada ya kufanikiwa kufika robo fainali, sasa tunatakiwa kupambana kupata matokeo mazuri ili kushinda mechi zote mbili ugenini na nyumbani kuweza kucheza nusu fainali ya michuano hii," alisema kocha huyo.

Baada ya mechi hiyo, timu hizo zitarudiana Jumamosi ya Mei 22, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na timu itakayopata matokeo ya jumla, itatinga nusu fainali ambapo itakutana na mshindi wa jumla kati ya Wydad Casablanca ya Morocco ama MC Alger ya Nigeria.

# Mbio CRDB Bank Marathon zapata usajili kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imetangaza kusajiliwa kimataifa kwa mbio zake za hisani za CRDB Bank Marathon, ambazo zilizozinduliwa mwaka jana kwa kauli mbiu ya "Kasi Isambazayo Tabasamu," zikilenga kuhamasisha kuchangia maendeleo na kusaidia wenye uhitaji katika jamii.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam katika hafla ya uzinduzi wa msimu mpya wa CRDB Bank Marathon 2021, Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Esther Mwambapa, amesema mapema mwaka huu mbio hizo zilipewa usajili wa kimataifa na Chama cha Usajili na Upimaji wa Mbio za Kimataifa (AMIS) kwa kushirikiana na Shirikisho la Kimataifa la Mchezo wa Riadha (World Athletics).

"Ninafuraha kuwajulisha kuwa mafanikio ambayo tuliyapata mwaka jana yamefungua milango kwa CRDB Bank Marathon kutambuliwa na kupata usajili wa kimataifa. Usajili huu wa kimataifa si tu unakwenda kupanua wigo wa kusambaza tabasamu, lakini unafungua fursa za kibiashara kwa Watanzania kwani tunatarajia wakimbiaji wengi wa kimataifa kujumuika nasi," aliongezea Tully huku akibainisha kuwa usajili huo wa kimataifa pia utasaidia kuitangaza Tanzania kimataifa.

Akielezea kuhusu msimu wa CRDB Bank Marathon 2021, Tully alisema lengo la mwaka huu ni kukusanya Sh. milioni 500 kusaidia gharama za upasuaji kwa watoto wenye matatizo ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI). Alisema pamoja na kuendelea kusaidia eneo hilo, sehemu ya fedha itakayokusanywa itapelekwa kusaidia ujenzi wa Kituo cha Huduma kwa Wateja "Call Centre" kwa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road.

"Kujisajili na kuchangia mbio hizi kwa binafsi ni shilingi 30,000 au kupitia vikundi ni 25,000. Malipo yanaweza kufanyika kupitia matawi ya Benki ya CRDB, CRDB Wakala, SimBanking App, mitandao ya simu na kupitia kadi ambazo zinawawezesha hadi watu wa nje ya nchi kufanya malipo," alisema Tully.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >